**Waziri:** Waandishi wanawake wapewe kozi za uongozi

UKURASA 4



**TBA** yatembeza operesheni kuondoa wadaiwa wao sugu

UKURASA 8



**DIARRA FITI KUIVAA AL AHLY**

UKURASA 20


# Nipashe

Alhamisi Novemba 30, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581600

www.ippmedia.com

www.twitter.com/ www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper




Basi la kampuni ya Ally's Star lenye namba za usajili T178 DVB, likinyanyuliwa na kreni kutoka kwenye njia ya reli baada ya kupata ajali ya kugonga kichwa cha treni wilayani Manyoni, mkoani Singida jana na kusababisha vifo vya watu 13 na kujeruhi 32. **PICHA: ELISANTE JOHN**

## Bibi harusi, mama yake wafa ajalini siku nne kabla ya sherehe

**Treni** na basi zaua 13, kujeruhi 32...

*Endelea ukurasa 2*

# CCM kwafukuta

UKURASA 2



Mkuu Mteule wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, akiongoza ibada ya kuaga mwili wa Askofu mstaafu wa kanisa hilo, Dayosisi ya Kaskazini, Dk. Erasto Kweka, katika Kanisa Kuu la Azania Front, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Malasusa: Askofu Kweka ameacha alama isiyofutika

UKURASA 3

UKURASA WA 2

### MALIPO KWA WAKALA YAIBUA TAHARUKI ZAHANATI, WATENDAJI WAKE WAKOSA MAJIBU

WAGONJWA katika Zahanati ya Serikali ya Tegeta, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, wamelalamikia mfumo mpya wa malipo ya huduma za afya kupitia wakala kuwa unachelewesha kupata matibabu na kukatwa fedha.

Juzi asubuhi, Nipashe ilifika katika ...

UKURASA WA 4

### POLISI WATIWA MBARONI MADAI KUUA KWA RISASI



JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia askari polisi wawili kwa tuhuma za kumpiga risasi raia na kumsababishia kifo eneo la Sinza Mapambano, Wilaya ya Kinondoni. Kaimu Kamanda wa Kanda hiyo, Gabriel Puppa, katika taarifa yake jana kwa...

**MICHEZO** **WACHEZAJI SIMBA WAWEKWA KITIMOTO** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# CCM kwafukuta

**Na Mwandishi Wetu**

NI rasmi Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo amejiuzulu, huku kitendawili cha anayerithi kiti chake kikibaki katika giza nene hadi jana usiku.

Uthibitisho wa ombi la Chongolo kujiuzulu, umekuwa wazi ukisindikizwa na Mwenyekiti wake, Rais Samia Suluhu Hassan kuridhia, hivyo ameondoka rasmi kwenye kiti hicho.

"Dk. Samia Suluhu Hassan ameijulisha Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kupokea barua ya kujiuzulu kwake, na ameridhia ombi hilo," alitamka Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Paul Makonda jana saa mbili usiku.

Makonda aliwafahamisha waandishi wa habari, kauli rasmi ya kwanza iliyofuta 'ukweli na uongo' wa tetesi zilizozagaa kuhusu Katibu Mkuu huyo.

Ni taarifa iliyotolewa kukiwa na minong'ono iliyotawala hadi jana usiku, kwamba wateule wa kumrithi Chongolo walikuwamo makada maarufu, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, Mzee John Chiligati na Abdallah Bulembo.

Makonda alisema Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa ilifanya kikao cha kawaida jana jijini Dar es Salaam chini ya Mwenyekiti, Rais Samia.

Alisema kuwa pamoja na mambo mengine, kikao hicho kilijadili hali ya kisiasa ndani ya chama na nje ya chama nchini.

Makonda alisema kikao hicho pia kilifanya uteuzi wa mwisho wa wagombea wa nafasi za uongozi ndani ya chama kwa ngazi ya mkoa na wilaya ili kujaza nafasi zilizoachwa wazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kifo na uteuzi wa nafasi nyingine.

Kwa mujibu wa Makonda, nafasi ya Mwenyekiti wa Mkoa wa Arusha, waliojitokeza wanachama 89, lakini walioteuliwa ni Dk. Daniel Pallangyo, Loy Sabaya, Solomon Kivuyo na Edna Kivuyo.

Mkoa wa Mbeya waliojitokeza 48. Walioteuliwa ni: Felix Iyaniva, Patrick Mwalunenge na Fatuma Kasenga. Mkoa wa Mwanza waliojitokeza 109. Walioteuliwa ni Michael Masanya, Sabana Salinja, Dk. Anjelina Samike, Elizabeth Nyingi na David Mulungo.

Makonda alisema kikao hicho pia kimeipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025.




Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kongamano la wanawake wafanyabiashara Afrika linalotarajiwa kufanyika kuanzia Desemba 6 hadi 8 mwaka huu katika jiji hilo. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Hashil Abdallah. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bibi harusi, mama yake wafa ajalini siku nne kabla sherehe

**Na Waandishi Wetu**

WATU watatu wa familia moja, akiwamo bibi harusi mtarajiwa, Rehema Chao (35), mkazi wa Morogoro na Mwalimu wa Shule ya Sekondari SUA, wamefariki dunia katika ajali ya gari iliyohusisha Toyota Raum na lori la mizigo aina ya Scania.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro, Abdalah Mwaipaya, aliiambia Nipashe jana kwa njia ya simu kuwa bibi harusi huyo alikuwa anaendesha gari hilo (Raum) kutoka Morogoro kwenda nyumbani kwao Msae-Marangu ili kuwahi harusi yake iliyokuwa ifungwe Jumamosi jijini Arusha.

Kwa mujibu wa Mwaipaya, wengine waliofariki dunia kutokana na ajali hiyo ni mama mzazi wa bibi harusi huyo, Agness Chao (75) na mfanyakazi wa ndani aliyemtaja kwa jina moja la Irene (19).

"Hiyo ajali imetokea usiku wa Novemba 29 mwaka huu, majira ya saa saba usiku katika Wilaya yetu ya Mwanga, eneo la Kisangara.

"Bibi harusi huyo ambaye alikuwa dereva wa gari hilo, alikuwa anakwepa shimo lililoko katikati ya barabara na ghafla alijikuta ameingia upande wa lori lililokuwa linakuja mbele yake na kugongana uso kwa uso," alisema.

Mkuu wa Wilaya alisema miili ya watu hao imehifadhiwa katika Kituo cha Afya Kisangara na majeruhi wawili wa ajali hiyo wanapatiwa matibabu Hospitali ya Wilaya ya Mwanga (Usangi).

**TRENI, BASI**

Wakati hayo yakijiri wilayani Mwanga, watu 13 wamefariki dunia na wengine 32 kujeruhiwa katika ajali iliyohusisha basi la kampuni ya Ally's Star lenye namba za usajili T178 DVB Golden Dragon, likitokea jijini Dar es Salaam kwenda Mwanza, kugonga injini ya treni kwenye makutano ya barabara kuu ya Manyoni - Singida, eneo la Manyoni mjini saa 10 alfajiri usiku wa kuamkia jana.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Stella Mutabihirwa, alisema tukio hilo limetokea wakati dereva wa basi hilo akijaribu kukatiza njia ya reli eneo la Manyoni mjini bila ya kuchukua tahadhari na hatimaye kugonga kichwa cha treni, mali ya Shirika la Reli (TRC). Namba za usajili: V951 9006.

Kwa mujibu wa Mutabihirwa, basi hilo likiwa katikati ya njia ya reli ghafla liligongwa na injini ya kichwa cha treni, kilichokuwa kinarudi Manyoni mjini kikitoka Kituo cha Stesheni Aghondi na kusababisha vifo na majeruhi. Wote ni abiria waliokuwa kwenye basi la Ally's Star.

Kamanda Mutabihirwa alisema basi hilo lilikuwa na jumla ya abiria 57 na waliofariki dunia ni 13, huku majeruhi wakiwa 32. Abiria wengine walionusurika na ajali hiyo, waliendelea na safari kwa kutumia magari mengine.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Dk. Furaha Mwakafwila, alithibitisha vifo hivyo 13 na kupokea majeruhi 32, baadhi ya majeruhi walipewa rufani kwenda Hospitali ya St. Gaspar Itigi, wilayani Manyoni na baadhi walitarajiwa kupatiwa rufani kwenda Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, aliongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa hadi eneo la tukio ambako aliwataka madereva kuzingatia sheria za barabarani.

Serukamba alieleza kusikitishwa na ajali hiyo na aliwatembelea na kuwapa pole majeruhi waliolazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni na waliopata rufani kwenda Hospitali ya St. Gaspar Itigi.

Taarifa iliyotolewa jana na TRC kupitia Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano, Jamila Mbarouk, ilieleza kuwa kati ya watu 13 waliofariki dunia, wanawake ni sita.

Miongoni mwa waliotajwa kufariki dunia kutokana na ajali hiyo ni mfanyakazi wa Upendo Media, Ruth Helson.

***Imeandaliwa na Mary Mosha (MOSHI) na Elisante John (MANYONI)**

## Malipo kwa wakala yaibua taharuki, zahanati yahojiwa na kukosa majibu

**Na Waandishi Wetu**

WAGONJWA katika Zahanati ya Serikali ya Tegeta, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, wamelalamikia mfumo mpya wa malipo ya huduma za afya kupitia wakala kuwa unachelewesha kupata matibabu na kukatwa fedha.

Juzi asubuhi, Nipashe ilifika katika zahanati hiyo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wagonjwa kuwa wamekuwa wakitumia muda mrefu katika malipo kwa kuwa wakala wanaotumika ni wa nje.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Kinondoni, Dk. Samwel Laizer, alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia malalamiko hayo, alisema huo ni utaratibu wa kawaida wa wagonjwa kulipia huduma za matibabu kwa kupatiwa namba ya malipo (control mumber).

Mgonjwa Mrisho Abdallah aliyekutwa akisubiri huduma katika zahanati hiyo alisema mfumo huo wakulipia mtandaoni unaleta shida kwao.

"Kama unavyoona mpaka sasa mawakala hawajafungua ofisi zao huko nje. Je, tutakaa na maumivu yetu mpaka saa ngapi? Pia jambo lingine tukifanya malipo kwa njia ya mtandao kama wanavyotaka tunakatwa makato," alidai.

Betha Fredrick, mkazi wa Tegeta, alisema alifika mapema kituoni hapo lakini wakala wa malipo alikuwa hajafika na kulazimika kumngojea.

"Unafika kituo cha afya unaumwa bado unalazimika kukaa kungojea wakala ili ufanye malipo kwa sababu huwezi kutibiwa bila kulipia. Pia unalipia matibabu bado unakatwa fedha za makato. Tunaomba hili liangaliwe upya," alisema.

Jonas Yusufu alisema mfumo huo kwa wagonjwa au kwa watu wenye mahitaji maalum ni mgumu na unahatarisha maisha kwa kuwa mgonjwa anakuwa hapati huduma kwa wakati.

Katika ufafanuzi wake, Dk. Laizer alisema inawezekana wakati huo mtandao ulikuwa unasumbua kwa kuwa huo ni utaratibu wa kawaida wa malipo.

"Ni utaratibu wa kawaida, lazima mwananchi alipe kwa kutumia namba ya malipo, huo sio mradi wa mtu binafsi serikali imeagiza watu walipe kupitia mfumo huo.

"Leo (jana) ukienda huwezi kukuta tatizo. Ni vitu ambavyo katika uendeshaji wa jambo vinatokea kwa mfano ukienda benki kuna muda unaambiwa mfumo hauko sawa. Mfumo huo umeanza Oktoba, mwaka huu, ndiyo maana unaonekana kama jambo geni. Lengo ni kuhakikisha fedha za serikali zinakwenda katika mfumo rasmi," alifafanua.

Alisema kwa mgonjwa wa dharura anapofika hospitalini hapo huwa hawasubiri mpaka alipe, uhudumiwe kwanza ndipo utaratibu wa malipo unafanyika.

"Kwa sasa tunaendelea kujipanga kuhakikisha tunamaliza vikwazo vyote tunapohudumia wananchi, lakini hakukua na taharuki yoyote," alisisitiza.

**•Imeandikwa na Tuntule Swebe na Halfan Chusi**

HABARI KITAIFA

# Malasusa: Askofu Kweka ameacha alama isiyofutika

**Na Beatrice Shayo**

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP), Dk. Alex Malasusa, amesema Askofu Mstaafu wa Dayosisi ya Kaskazini, Dk. Erasto Kweka, ataendelea kuishi katika mioyo ya Watanzania kutokana na mchango mkubwa alioutoa kiroho na kimwili.

Malasusa amesema Askofu Dk. Kweka katika uhai wake hasa katika kipindi chake cha uongozi wa dayosisi hiyo, alifanya mambo makubwa katika elimu na afya huku akisisitiza watu kujikomboa kiuchumi na kuwataka watumishi kuondokana na dhana ya kuwa ombaomba.

Askofu Dk. Malasusa alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akiongoza ibada ya kumuaga Askofu Dk. Kweka aliyefariki Novemba 25, mwaka huu, katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) alikokuwa anapatiwa matibabu. Mwili wa kiongozi huyo utazikwa Desemba 6, mwaka huu, katika Usharika wa Uswaa, Hai mkoani Kilimanaro.

Malasusa ambaye ni Mkuu Mteule wa KKKT, alisema Askofu Kwema alikuwa ni mtu wa kazi tena aliifanya kwa bidii.

"Tumeambiwa alifundisha mambo ya uchumi na kutaka kila mmoja awe na uchumi hasa wachungaji.

Aliwataka wachungaji kuacha kuwa ombaomba na alisisitiza kuwa mchungaji si tiketi ya kuwa ombaomba na anafanya kazi kujiinua kiuchumi. Hiki ndicho ambacho alikitofautisha na sisi wa leo. Yeye mwenyewe hakupenda kuwa ombaomba, alifanya kazi mwenyewe," alisema.

"Kwa sasa hivi tabia hii (ya kuwa ombaomba kwa watumishi wa kanisa) inakua sana na kufikiri kwamba unapokuwa mtumishi wa Mungu basi una haki ya kunyoosha mkono tu lakini kumbe ukiwa mtumishi wa Mungu, una haki pia ya kuingiza mkono mfukoni na kunyoosha kwa maskini. Baba Askofu Kweka alikuwa na roho hiyo," aliongeza.

Dk. Malasusa alisema watu wanatafsiri sadaka wanavyoweza kwa sasa ili iwe faida kwao hilo lilikuwa tofauti kwa Askofu Kweka.

"Alitaka kuifanya kazi kwa mikono yake mwenyewe. Unajua kuna watu wana fedha kwa sasa hivi tunaweza kuwalaumu kwa nini hawaji kanisani kwa sababu labda wanaogopa kuombwa ombwa.

"Askofu Kweka alifanya kazi mwenyewe, akaondoa dhana ya kwamba mtumishi wa Mungu ni maskini. Yeye alisimama katika dhana kwamba Mungu nipe mkate wangu wa kila siku, ataula yeye na familia," alisema.

Kutokana na mtazamo huo, Askofu Malasusa alisema angetamani watu wajifunze dhana ya utumishi kwa kuwa Paulo (kwa mujibu wa maandiko matakatifu) alisema asingependa kuwalemea wengine kwa ajili ya injili. Alisema unayepata wito wa injili uibebe mwenyewe.

"Siku hizi kuna mafundisho mengi ya utajirisho lakini Askofu Kweka yeye alifundisha zaidi uchumi na wapo wengi ambao wameyaiga kutoka kwake. Kwa hilo sisi watumishi tutaendelea kumuenzi.

"Lakini baba huyu pamoja na yote ambayo Mungu amempa na vipawa vingi na kujulikana ndani na nje ya nchi, bado aliishi kama mnyenyekevu kuliko jina lake lilivyotukuka. Siku hizi watu wanapanda kidogo, unyenyekevu unakuwa F lakini Baba Askofu aliendelea kuishi katika unyenyekevu.

"Askofu Kweka alijenga jina lake, hakuwa mtu mwenye mizaha mizaha na wengine walishindwa kumfahamu kwa sababu maisha ya sasa watu wanaishi kwa mazoea. Jambo lingine Askofu Kweka alikuwa mtu mwaminifu. Ni wale wachache ambao wanajua alipata neema ya kujua wokovu mapema kuliko watu wanavyofikiri.


"Tunamshukuru Mungu kwa kutuletea Askofu huyu ndani ya kanisa letu. Licha ya kuwa kiongozi wa watu, alijinyenyekeza kwa Mungu. Mara nyingine unapokuwa na watu wengi wanaokushabikia ni rahisi sana kumsahau Mungu. Napenda niwashuhudia siku zote, Askofu Kweka aliifanya nyumba yake kuwa nyumba ya bwana," alisema.

Malasusa alisema kupitia Maisha ya Askofu Dk. Kweka, Mungu anatamani wanadamu kuishi kwao waache alama kwa tumtumikie Mungu kwa nguvu bila kujali hali zao na nafasi zao.

"Mungu anataka sisi pia tuishi kama watu wenye ushuhuda si tu kushangaa. Tujitahidi kubadilika kwani haitoshi kuumia, kusikitisha au kuwa na historia kubwa. Baba Askofu Kweka amemaliza, sasa kazi imebaki kwetu na sisi tuwe tayari kumtumikia Mungu," alisisitiza.

Msemaji wa familia, Dk. Kumbaeli Salewi, aliushukuru uongozi wa DMP kwa msaada mkubwa waliopatiwa wakati wote tangu Askofu Kweka alipokuwa akitibiwa JKCI hadi mauti yalipomkuta na hatimaye kumsafirisha Kwenda Kilimanjaro.

"Familia tumefarijika kwa namna kanisa lilivyojitoa tangu alivyokuwa anaumwa hadi sasa. Wametushika mkono tunawashukuru wote waliotukimbilia," alisema.




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 29/11/2023

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Ijumaa tarehe 01-12-2023** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea MTWARA,** gari hilo lenye namba za usajili: **T 176 DFN / T 171 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **18.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.80** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.00** |

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM hadi MTWARA** kupitia **KILWA ROAD.** Gari itasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



**LINDI FORESTS LIMITED**
The companies Act, 2002 (Section 345)

**MEMBER'S VOLUNTARY WINDING – UP**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN** to the general public that **LINDI FORESTS LIMITED** a company with registration number **54989** dully intends to convene a final meeting on 30th December, 2023 in accordance to section 345(2) of the Companies Act, 2002. The purpose of the general meeting is laying before the accounts and giving any explanation thereof.

All parties concerned and who have claims are hereby called to attend the meeting at **Basil & Alred office, Ace Building (1st Floor), Haile Selassie Road, Dar es salaam, Tanzania on 30th December, 2023 at 10am.**

**GODFREY BASIL MRAMBA**
**Liquidator**
**For LINDI FORESTS LIMITED**

177345



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
30.11.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Ijumaa tarehe **01-12-2023 hadi 03-12-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Mzenga**, gari hizo zina namba za usajili: **T 203 DYJ /T 393 DVS T 204 DYJ / T 394 DVS T 896 DSD / T 416 AYQ T 163 DFC / T 321 DDH**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 23.00** |
| **Upana** | - | **mita 4.50** |
| **Kimo** | - | **mita 5.00** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam Port, hadi Mzenga kupitia Mlandizi**, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
30.11.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Ijumaa tarehe 01-12-2023** hadi **03-12-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Mzenga,** gari hizo zina namba za usajili: **T 289 EDD / T 387 DHQ T 468 DYG / T 310 DDH T 295 EDD / T 390 DHQ T 167 DFC / T 777 AQR**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 23.00** |
| **Upana** | - | **mita 7.40** |
| **Kimo** | - | **mita 4.80** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam Port, hadi Mzenga kupitia Morogoro Road** Gari zitasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** kutoka **Dar-Es-Salaam Port mpaka Mlandizi** Kutoka Mlandizi Kwenda Mzenga gari itasafiri muda wa mchana ***(Kuanzia saa12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

# Waandishi wanawake wapatiwe kozi maalum ya uongozi - Waziri

**Na Beatrice Moses**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera - Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, amependekeza kuwekwa utaratibu wa kuwapa kozi za uongozi waandishi wa habari wanawake ili kuwajengea uwezo wa kuwa viongozi kwenye vyumba vya habari.

Aliyasema hayo jana alipomwakilisha Mgeni Rasmi, Rais Samia Suluhu Hassan kwenye kilele cha Maadhimisho ya Miaka 36 ya Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Waziri huyo alisema Mamlaka ya Elimu (TEA) na Uongozi Institute wanaandaa kozi hizo maalum kwa mpangilio mzuri wa mafunzo hayo kwa waandishi wa habari wanawake, hatua ambayo itawafanya kuwa viongozi wazuri zaidi.

Alisema viongozi wengi wanawake ni waaminifu na ni waoga kufanya uhalifu, hivyo wanapaswa kuaminiwa hasa kama sifa zinazohitajika kwenye nafasi husika ya uongozi.

"Kuupata uongozi ni jambo moja, lakini kuulinda ni kazi kubwa. Kazi yetu ni kuulinda uongozi ili kusaidia wanawake wengine kuingia kwenye nafasi za uamuzi," alisema.

Aliwataka wanawake wanaopata nafasi ya kuwa kwenye uamuzi, wahakikishe wanatendea haki nafasi hizo ili kuendelea kuiondoa dhana potofu ya kufikiri wanawake hawawezi uongozi.

Waziri Jenista alisema kupinga mfumo dume haimaanishi kuvunja heshima ya mwanamume bali ni kutaka mfumo uliosawa kwenye mfumo wa maisha ya maendeleo ikiwamo elimu, uongozi na umiliki wa mali.

"Kuna wanaume wanaposikia usawa wa kijinsia wanadhani inawahusu wanawake tu, wakati suala la jinsia linahusu jinsi mbili; ke na me na tunapokwenda kuvunja mifumo dume haimaanishi kupambana na wanaume.

"Tutumie siku hii kusheherekea miaka 36 ya TAMWA kwa kulinda na kuthamini haki za wanawake na watoto, kuendeleza maadili ya Mtanzania na kupinga ukatili wa kijinsia," alisema.

Waziri huyo alisema Rais Samia anawapongeza TAMWA na anaamini kati ya taasisi zenye mchango katika kukuza usawa wa kijinsia, TAMWA ni miongoni.

Mwenyekiti wa TAMWA, Joyce Shebe alisema katika kuadhimisha miaka 36 ya TAMWA, kuna mambo kadhaa yanayojitokeza ikiwamo mafanikio na changamoto katika utekelezaji majukumu yao ikiwamo kutetea usawa wa kijinsia, kumkomboa mwanamke dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Alisema tatizo la rushwa ya ngono kwenye vyombo vya habari bado ni kubwa, akilitaja kukwaza jitihada za kupambana na ukatili huo wa kijinsia, hivyo inatakiwa kuchukua hatua stahiki.

"Tatizo la rushwa ya ngono ni kubwa na limekuwa vikwazo kwa wasichana kufikia ndoto zao. TAMWA tumejikita kutoa elimu ili kupambana na rushwa hii," alisema.

Jarida maalum la Sauti ya Siti linaloelezea kuhusu wanawake waliokumbwa na rushwa ya ngono na uelimishaji wa madhara ya vitendo hivyo limezinduliwa.

Alisema TAMWA imekuwa mstari wa mbele kutoa matamko ya kupinga ukatili wa kijinsia na serikali kuchukua hatua kudhibiti vitendo vya ukatili kama vile mauaji ya albino na wazee vikongwe."

Shebe alisema TAMWA imefanikiwa kutetea haki za wanawake, watoto na wenye mahitaji maalum, hatua iliyowatia moyo kwa kuwa ni moja ya mafanikio kwa kazi walizokusudia kuzifanya.

Maadhimisho hayo yamehudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu, Celestine Kakere na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo, Msemaji Mkuu wa Serikali Mobhare Matinyi, wabunge wanawake kutoka Kenya na wawakilishi wa mashirika mbalimbali ya maendeleo na asasi za kiraia.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama, akiangalia gazeti la Nipashe lililoshikwa na Mhariri Mtendaji wa Gazeti hilo, Beatrice Bandawe, alipotembelea maadhimisho ya miaka 36 ya Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Chama hicho, Joyce Shebe. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Muhimbili yafanya upasuaji wa kuweka nyonga, magoti bandia

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili - Mloganzila kwa kushirikiana na Taasisi ya Global Medicare, wamefanya upasuaji wa kuweka magoti na nyonga bandia kwa wagonjwa 14.

Upasuaji huo umefanyika katika kambi maalum hospitalini huko iliyoanza Novemba 27 na inatarajiwa kumalizika kesho. Wagonjwa 35 wanatarajiwa kufanyiwa upasuaji.

Akizungumza na waandishi wa habari hospitalini huko jana, Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Upasuaji wa hospitali hiyo, Dk. Godlove Mfuko, alisema kufanyika operesheni hiyo kunadhihirisha namna Mloganzila ilivyokidhi viwango vya kimataifa vya kufanya aina hiyo ya upasuaji.

"Kwa viwango vya kimataifa mtu aliyefanyiwa aina hii ya upasuaji kama hakuna dharura yoyote huwa ni siku tatu hadi tano anakuwa ameruhusiwa, na sisi tunakwenda na viwango hivyo ambapo wagonjwa walifanyiwa Jumatatu leo (jana) wanaruhusiwa," alisema.

Dk. Mfuko alibainisha kuwa mbali na kupata wagonjwa kutoka mikoa yote ya Tanzania, pia kuna mgonjwa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), jambo linaloonyesha kuwa kambi si tu imenufaisha Watanzania, bali pia raia kutoka mataifa mbalimbali.

Kiongozi wa kambi hiyo, Prof. Mamoun Gadir kutoka Hospitali ya Queen Elizabeth ya Uingereza, alisema mpangilio na muundo wa Hospitali ya Mloganzila hauna tofauti na hospitali za nchi zilizoendelea.

Alisema wataalamu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila wanayo maarifa na ujuzi wa kimataifa, kwamba wanahitaji kuongezwa maarifa ya ziada ili wawe wabobezi wakubwa.

Aliishauri Hospitali ya Mloganzila kuwa na kituo maalumu cha kutoa matibabu ya nyonga na magoti.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Nyonga na Magoti MNH-Mloganzila, Shilekilwa Makira alitaja mambo yanayosababisha maradhi ya nyonga na magoti ni pamoja na umri mkubwa, maradhi ya selimundu, pumu ya mifupa na ajali.

Alisema kambi hiyo mbali na kutoa huduma, pia imetoa fursa kwa wataalamu kutoka Hospitali ya Rufani Temeke, Hospitali ya CCBRT na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya (MZRH) kujifunza.

Alitoa shukrani kwa wataalamu wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) kwa kushiriki kuwajengea uwezo.

Dk. Makira alisema: "Baada ya kambi kuisha utaratibu wa matibabu kwa watu wenye matatizo ya nyonga na magoti utaendelea kama kawaida. Tutawaona katika kliniki zetu na kama wataonesha wanahitaji upasuaji tutawafanyia."

# Polisi watiwa mbaroni madai kuua kwa risasi

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia askari polisi wawili kwa tuhuma za kumpiga risasi raia na kumsababishia kifo eneo la Sinza Mapambano, Wilaya ya Kinondoni.

Kaimu Kamanda wa Kanda hiyo, Gabriel Puppa, katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari, alibainisha kuwa jeshi hilo jana lilipokea taarifa hiyo ya kuwapo tukio hilo.

Alisema watuhumiwa hao wanadaiwa kumjeruhi kwa kumpiga risasi Razaki Azan (29) ambaye ni mlinzi binafsi wa baa ya Board Room iliyoko Sinza, ambaye baadaye alipoteza maisha.

"Jeshi la Polisi tayari limewakamata askari hao na mambo ya kisheria yanakamilishwa na watachukuliwa hatua za kisheria haraka kadri iwezekanavyo kwa kufuata mifumo ya kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani," alisema.

Kaimu Kamanda huyo alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala.

**Alisema watuhumiwa hao wanadaiwa kumjeruhi kwa kumpiga risasi Razaki Azan (29) ambaye ni mlinzi binafsi wa baa ya Board Room iliyoko Sinza, ambaye baadaye alipoteza maisha.**

# Ndalichako aona tija kuadhimisha Siku ya Watu Wenye Ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Watu Wenye Ulemavu Duniani yatakayofanyika kitaifa kwa mwaka huu mkoani Dodoma Desemba 2, mwaka huu.

Prof. Joyce Ndalochako, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

"Tunaendelea kuhamasisha watu wenye ulemavu wawezeshwe kwa kuwa wamekuwa wanafanya vizuri, kikubwa ni kuwaandalia mazingira na kuondoa vikwazo," alisema.

Waziri huyo alisema maadhimisho hayo yanatumika kama daraja kwa watu wenye ulamavu nchini kujadili changamoto zinazowakabili, kuleta ustawi wa jamii, kupata tathmini na kutoa huduma.

Alisema maadhimisho hayo pia yanatumika kuhamasisha jamii kutambua haki za walemavu na jinsi ya kutatua changamoto zinawakabili.

Alisema wakati wa maadhimisho hayo, huduma mbalimbali zitatolewa ikiwamo uchunguzi wa afya utakaofanywa na madaktari bingwa.

Kwa mujibu wa Prof. Ndalichako, maadhimisho hayo yatakuwa na maonyesho ya bidhaa zinazotengenezwa na watu wenye ulemavu ambao ni wajasiriamali na kilele chake kitatanguliwa na maandamano.

Alisema maofisa ustawi wa jamii na maofisa elimu maalum watajumuishwa katika maadhimisho hayo na kuwataka kuwawezesha watu wenye ulemavu kwenye mikoa yao kushiriki.

Pia alizitaka familia kuambatana na ndugu zao wenye ulemavu katika maadhimisho hayo na kuachana na mila potofu ambazo zimekuwa zinasababisha watengwe.

Katibu wa Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu Wanawake na Watoto Tanzania, Mzawa Jagama, aliishukuru serikali kwa kuwatambua, kuwajali watu wenye ulemavu, kuwapa faraja na amani.

Awali Prof. Ndalichako aliwafariji wafanyakazi waliopata ulemavu wakiwa kazi wanaopatiwa mafao na Mfuko wa Fidia wa Wafanyakazi (WCF) katika ofisi za mfuko huo jijini Dar es Salaam.

# Mwanafunzi ahitimu udaktari na miaka 21

**Na Joseph Mwendapole**



MWANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu cha Hurbert Kairuki (HKMU), Ahlam Azam Mohamed, ameweka rekodi ya kuwa mwanafunzi mdogo kuliko wote kuwahi kutokea nchini kuhitimu shahada ya udaktari wa binadamu akiwa na umri wa miaka 21.

Mwanafunzi huyo atakuwa miongoni mwa wahitimu 138 wa fani ya udaktari katika mahafali ya chuo hicho yatakayofanyika keshokutwa.

Makamu Mkuu wa HKMU, Prof. Yohana Mashalla, alisema jana kuwa wameangalia rekodi mbalimbali nchini na hawajaona mtu aliyewahi kuhitimu fani ya udaktari binadamu kwa umri huo.

"Tumeuliza kwenye vyuo mbalimbali vya tiba kuona kama kuna mtu aliyewahi kuhitimu shahada ya udaktari kwa umri wa miaka 21 kikiwamo Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi za Tiba Muhimbili (MUHAS) lakini wamesema haijapata kutokea. Kwa hiyo tunampongeza Ahlam kwa kuweka rekodi," alisema.

Prof. Mashalla pia alisema HKMU imemaliza tathmini ya utekelezaji wa mpango mkakati wa chuo wa miaka mitano wa 2018-2023 na mwezi huu kilizindua mpango mkakati wa miaka mitano ijayo.

Alisema mpango huo umejikita katika maeneo ya kimkakati sita ambayo ni uimarishaji wa utoaji wa elimu na utawala ikiwa ni pamoja na kimazingira ya kufundishia na kuongeza udahili, kuboresha mtandao na kuongeza matumizi ya teknolojia katika utoaji wa elimu kwa wanafunzi, wanataaluma na wafanyakazi.

Prof. Mashalla pia alisema kwenye mpango mkakati huo, chuo kimepanga kuongeza utafiti, machapisho, ubunifu na kuimarisha mifumo ya mipango na fedha.

Alisema katika kutekeleza mpango huo mwaka huu wa masomo chuo kimedahili wanafunzi wapya 465 katika fani mbalimbali.

"Ongezeko hili la wanafunzi katika mwaka wa kwanza litafanya chuo kuwa na jumla ya wanafunzi 1,628 kulinganisha na wanafunzi 1,452 katika mwaka wa masomo uliopita," alisema.

Katika mahafali ya mwaka huu, wahitimu watakuwa 296 na kati yao wanawake ni 166 na wanaume ni 130 wakati kwenye shahada ya udaktari wa binadamu wanawake ni 65 na wanaume ni 73.

Profesa Mashalla alisema kabla ya mahafali hayo, kutakuwa na kusanyiko la kitaaluma ambalo litajadili fursa za kibiashara na mgeni rasmi atakuwa aliyewahi kuwa Naibu Waziri wa Fedha, Janeth Mbene.

"Tumeona badala ya kujadili masuala ya afya peke yake tuite wataalamu wabobezi kwenye masuala ya biashara na uchumi ili nao watoe mchango katika utoaji wa wataalamu kwenye sekta ya afya," alisema.




Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini, Mrisho Gambo (kushoto), akionyesha kwa waandishi wa habari, baadhi ya vifaa vya matibabu ikiwamo X-ray ya kidijitali, gari la kubebea wagonjwa na mashine mpya ya CT-Scan, vilivyotolewa na serikali katika Hospitali ya Rufani Mt. Meru jijini Arusha jana. Kulia ni Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Alex Ernest. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Kanisa lashukuru kusafishwa kuhusu tuhuma za jinsia moja

**Na Romana Mallya**

ASKOFU wa Jumuiya ya Kidini ya Spirit Word Ministry (SWM), iliyoko Stakishari, Dar es Salaam, Dk. Ceasar Masisi, ameishukuru serikali baada ya kukamilisha uchunguzi dhidi ya tuhuma zilizokuwa zikilikabili kanisa lao.

Uchunguzi uliokuwa ukifanywa ulihusisha madai ya kanisa kutoa mahubiri na mafundisho yenye mwelekeo wa kuhamasisha vitendo vya mapenzi ya jinsia moja.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini humo, Askofu Masisi alisema baada ya uchunguzi uliofanywa na serikali, wamepokea taarifa ya uamuzi unaowaondolea katika shutuma na hatia hiyo.

"Serikali yetu, chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, imetenda haki dhidi yetu. Uchunguzi umeonyesha kwamba hatuna hatia. Ni mitandao ya kijamii ilipotosha ukweli kwani ilionyesha tu sehemu ndogo ya video kutoka video kuu ilikatwa na kusambazwa ili kuhalalisha tuhuma ambazo sasa zimedhihirishwa hazikuwa za kweli," alisema.

Mei 29, mwaka huu, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, akisoma Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa mwaka wa fedha 2023/24 bungeni jijini Dodoma, alisema wamesitisha usajili wa jumuiya hiyo baada ya kubaini kutoa mahubiri na mafundisho yenye mwelekeo wa kuhamasisha vitendo vya mapenzi ya jinsia moja.

Alisema katika kudhibiti na kupambana na vitendo hivyo vya mmomonyoko wa maadili Ofisi ya Msajili wa Jumuiya imesitisha shughuli ya kidini ya jumuiya hiyo.

Juzi, Askofu Masisi alisema serikali ni kama baba katika familia, wakati wote yupo tayari kuinusuru familia yake kwenye hatari yoyote anayoona ipo mbele ya familia yake.

Alisema serikali katika kipindi cha uchunguzi ilichukua hatua kadhaa kama baba, ikiwa pamoja na msajili kusimamisha huduma za kanisa lao, kufunga ukumbi wa kukutania na baadaye kufuta usajili wa kanisa.

"Mambo hayo yote yalitokea kwa kipindi cha muda mfupi sana, na baada ya miezi sita, Jeshi la Polisi lilitoa majibu ya uchunguzi wao kwamba hatuna hatia dhidi ya tuhuma zile," alisema.

Pamoja na majibu waliyopewa, pia alisema walipokea barua ikiwataka jengo lao lifunguliwe na kutumika kwa shughuli nyinginezo za kijamii na sio huduma za kanisa, kwa vile msajili alishafuta huduma zilizokuwa zikitolewa hapo mwanzo.

"Hii ni changamoto kubwa kwetu pamoja na waumini wote wa SWM. Kilio chetu mbele ya serikali yetu sikivu na makini ni juu ya kutupa ruhusa tena kuendelea kumwabudu Mungu wetu pasipo hofu wala wasiwasi.

"Tunaishukuru serikali yetu kwa kusimamia haki, na kwa dhati, tunatoa tamko la kuwa hatuna uhusiano wowote na wale wanaotetea mapenzi ya jinsia moja," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mfumo huu malipo mtandao matibabu usitese wagonjwa

**KATIKA** kuhakikisha mianya ya upotevu wa mapato katika nyanja mbalimbali serikalini unadhibitiwa, ulianzishwa utaratibu wa malipo kwa njia ya kielektroniki na kupitia mitandao ya simu au benki.

Hatua hiyo ilichukuliwa baada ya kuonekana kuwa wajanja wachache wakiwamo watumishi wa serikali katika serikali kuu na mamlaka za serikali za mitaa pamoja na mawakala waliopewa zabuni za kukusanya mapato, kutumia mwanya wa kukusanya fedha nyingi na kuwasilisha kidogo katika sehemu husika. Jambo hilo lilisababisha malengo ya serikali katika ukusanyaji mapato kuwa kidogo, hivyo kufanya miradi mingi ya maendeleo kutokutekelezwa ipasavyo.

Katika mapato ya kodi yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), fedha zilizokuwa zikipatikana zilikuwa ndogo kulinganisha na uhalisia wa eneo husika. Hiyo ni kutokana na baadhi ya watumishi wa mamlaka hiyo wasio waaminifu kutumia mwanya kuiba fedha za umma.

Kwenye vivuko kama vile eneo la Feri, jijini Dar es Salaam, kulikuwa na kituko cha taarifa kilichotolewa kuwa kwa siku zinakusanywa si chini ya Sh. milioni mbili! Hata katika masoko makubwa kama vile Kariakoo na stendi ya mabasi yaendayo mikoani, maarufu kama Stendi ya Magufuli, Mbezi mkoani Dar es Salaam zinakusanywa kwa njia ya kielektroniki.

Hali hiyo ya kuvuja kwa mapato, ya kikodi na yasiyo ya kodi, ilisababisha serikali kuanzisha mifumo mbalimbali ya malipo ikiwamo ya kutumia mashine za kielektroniki (EFD), benki na mawakala. Kwa kiasi kikubwa, hatua hiyo ilisaidia mapato kuongezeka katika maeneo mbalimbali.

Malipo kwa mtandao na kupitia benki pia yameanzishwa katika vituo vya serikali vya afya yamesaidia kudhibiti wajanja kuchomoa fedha za serikali na wakati huo huo kuongeza ukusanyaji wa fedha kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Pamoja na hatua hiyo kuwa nzuri, katika baadhi ya maeneo ya vituo vya kutolea huduma za afya, kumekuwa na kero ambazo iwapo hazitafanyiwa kazi, zinaweza kuweka rehani maisha ya wagonjwa. Mfano wa kero hiyo ni Zahanati ya Tegeta, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, ambako wagonjwa wamelalamikia mfumo wa malipo ya huduma za afya kupitia wakala kuwa unachelewesha kupata matibabu.

Baadhi ya wagonjwa walitoa madukuduku yao kuwa wakifika katika zahanati hiyo kwa ajili ya matibabu, wamekuwa wakichukua muda mrefu kupata huduma. Sababu kubwa ni kwamba mawakala wa huduma za kifedha kwa njia ya mtandao wakati mwingine wamekuwa wakichelewa kufungua.

Huo ni mfano tu lakini inawezekana kuna maeneo mengi wananchi wamekuwa wakikumbana na kero hiyo lakini hawajafikiwa na kupaza sauti zao na hatimaye hatua kuchukuliwa na huduma kuboreshwa. Swali la kujiuliza ni kwa nini asiwapo wakala wa huduma za fedha mtandao pamoja na benki? Hiyo ifahamike kwamba mgonjwa hawezi kupatiwa huduma kabla ya malipo kusika kufanyika, hali ambayo inahatarisha maisha yake.

Ni vyema huduma hiyo ikapatikana ndani ya eneo la huduma ya afya kama inavyofanyika katika hospitali za mikoa kama Amana, Mwananyamala na Temeke ambako mgonjwa hata akifikishwa usiku wa manane hakumbani na adha kama hiyo.

Kutokana na kero hiyo, uongozi wa afya Manispaa ya Kinondoni umejaribu kujitetea kwamba kulikuwa na hitilafu ya kimtandao lakini ukweli ni kwamba mawakala wanaotoa huduma katika eneo hilo wanachelewa kufungua hatua ambayo inasababisha kero na mateso kwa wagonjwa na ndugu wanaowauguza.

Ni vyema viongozi wanaohusika wakaacha kutoa hoja za utetezi na badala yake wajaribu kutatua kero wanazopewa ili kuboresha huduma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Tujitafakari tunavyowakatili watoto, kuwakeketa, sasa jipya la maji moto!

**VITENDO** vya ukatili dhidi ya watoto, ni mojawapo ya matukio ambayo yanaendelea kujitokeza nchini kila kukicha na kusababisha maisha yao kuwa hatarini, iwapo hatua ya kuvidhibiti hazitachukuliwa haraka.

Chanzo cha kuwapo kwa vitendo hivyo, kimekuwa kikitajwa na baadhi ya watu kuwa ni mmomonyoko wa maadili, lakini kuwapo matukio hayo, huku wengine wakisema ni tatizo la afya ya akili.

Inawezekana majibu yote yakawa sahihi, lakini jambo la muhimu ni kurudi kwenye mstari kwa kuchukua hatua madhubuti ya kudhibiti vitendo hivyo ndani ya jamii, ili watoto waweze kuishi salama.

Serikali inakiri kwamba vitendo vya ukatili kwa watoto ni janga kwa taifa na inaahidi kuvivalia njuga na kupambana navyo ili kuvikomesha visiendelee kutishia maisha ya watoto.

Wakati serikali inaahidi kupambana na vitendo hivyo, ninadhani lisiwe jukumu la serikali tu katika vita hii, bali jamii nayo inahusika kwa kiasi kubwa ikiwamo kukomea na kutoa taarifa za vitendo hivyo.

Inasikitisha kusikia au kushuhudia, mtoto akichomwa kwa maji ya moto na mzazi wake, eti kisa kikiwa ni tuhuma za kuiba mboga. Maana yake ni kwamba mboga ni bora kuliko uhai wa mtoto!

Hilo ni tukio ambalo limetangazwa kwenye vyombo vya habari jana, lililotokea Tarime mkoani Mara na kusababishia mtoto maumivu makali kwenye mikono yake iliochomwa.

Wakati tukio hilo linatokea, takwimu zilizotolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum zinaonyesha kuwa kwa mwaka jana watoto 12,163 walifanyiwa ukatili.

Naibu Katibu Mkuu anafafanua kuwa 6, 365 kati ya hao, walibakwa, huku na kwamba kuna haja ya kufanya utafiti ambao utakuja na suluhisho la vitendo hivyo vinavyotishia usalama na maisha ya watoto.

**Serikali inakiri kwamba vitendo vya ukatili kwa watoto ni janga kwa taifa na inaahidi kuvivalia njuga na kupambana navyo ili kuvikomesha visiendelee kutishia maisha ya watoto.**

Pamoja na mbinu hizo za serikali, ninaamini kwamba suluhisho la vitendo vya ukatili kwa watoto ni wazazi na walezi kuzingatia malezi bora na jamii kushirikiana kuendelea kutoa elimu kuhusu madhara ya vitendo hivyo.

Vilevile wataalamu wa saikolojia, madaktari na wanasheria, wanapaswa kuwajibika au kupewa nafasi ya kushiriki kikamilifu kwenye vita hii dhidi ya vitendo vya ukatili, kwa kuwajengea watu uelewa juu ya vitendo hivyo na madhara yake.

Ninadhani ukatili huo, achilia wa kubakwa, wa mzazi kutoona tatizo kumchoma moto mtoto wake, kwa kosa ndogo la kuiba shilingi 100, kuiba mboga au wizi wowote, anayefanya vitendo hivyo anaweza kuwa na tatizo la afya ya akili kama ambavyo baadhi ya wataalamu wa saikolojia wanasema.

Kwa sasa, Tanzania imeungana na nchi nyingine duniani katika Kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto, kilele chake kitakuwa ni Desemba 10 mwaka huu.

Ingawa Tanzania inashiriki kampeni hizo kila mwaka, bado vitendo vya ukatili dhidi ya makundi hayo vinaendelea kuripotiwa, hivyo ni wazi kwamba kuna haja ya kuongeza kasi ya vita, hasa kwa kila mmoja kwa nafasi yake kushiriki.

Wizara yenye dhamana na watoto, iliandaa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008 inayoainisha haki tano za msingi za mtoto ikiwamo ya kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kushiriki na ya kutobaguliwa.

Kwa kuwa sera hiyo imeweka wazi haki za mtoto, ingekuwa ni vyema kama zingeheshimiwa ili kuondoa vitendo vya ukatili ambavyo wanakumbana navyo, huku wengine wakipoteza maisha au kuwa na ulemavu wa kudumu.

HABARI PICHA

# IBADA YA KUMUAGA ASKOFU MSTAAFU MAREHEMU DK. ERASTO KWEKA KATIKA KANISA LA KKKT AZANIA FRONT



Mkuu Mteule wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, akiongoza ibada ya kuaga mwili wa Askofu mstaafu wa kanisa hilo, Dayosisi ya Kaskazini, Dk. Erasto Kweka, katika Kanisa Kuu la Azania Front, Dar es Salaam jana. PICHA **ZOTE: MIRAJI MSALA**



Wachungaji na maaskofu wastaafu wakiimba nyimbo za maombolezo katika ibada hiyo.



Familia ya Askofu Dk. Kweka wakiwa katika ibada ya kumuaga mpendwa wao. Wa pili kushoto mbele ni mke wa marehemu, Shichanaisaria Kweka.



Sehemu ya waombolezaji waliohudhuria ibada ya kumuaga Dk. Kweka.




Askofu Dk. Malasusa na mke wa Marehemu, Shichanaisaria Kweka, wakitoa heshima za mwisho mbele ya jeneza lenye mwili wa Askofu Dk. Kweka.



Askofu Dk. Malasusa akiwa amemshika mkono Mama Shichanaisaria Kweka baada ya ibada kumalizika.

# Operesheni kuondoa kwa nguvu wadaiwa sugu wa TBA yaanza

**Na Halfani Chusi**

OPERESHENI ya kuhamisha wadaiwa sugu kwenye nyumba za serikali kwa Mkoa wa Dar es Salaam ilianza jana, Nipashe ikishuhudia wadaiwa sugu watatu waliokuwa wanaishi katika nyumba za Mbezi Chini wakihamishwa kwa usimamizi wa dalali wa mahakama kwa kushirikiana na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA).

Operesheni hiyo imeanza ikiwa ni siku chache baada ya serikali kupitia TBA kutangaza kuanza kuwaondosha kwa nguvu wadaiwa sugu kwa kutumia dalali wa mahakama kwa Mkoa wa Dar es Saalam. Watumishi hao wanadaiwa jumla ya Sh. bilioni 1.1.

Kaimu Meneja wa TBA Mkoa wa Dar es Salaam, Bernard Mayemba, alisema operesheni hiyo ni endelevu. Watazifikia nyumba zingine za serikali na hakuna mdaiwa sugu atakayeachwa kwenye nyumba hizo.

Alisisitiza mpangaji atakayehamishwa, atatakiwa kulipa deni analodaiwa. Akishindwa, atachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kupelekwa mahakamani.

"Mkoa wa Dar es Salaam una nyumba zaidi ya 1,200, lakini kumekuwa na tabia ya baadhi ya watumishi wa umma kutolipa kodi ya pango kwa wakati.

"Hatua hii kwa sasa haitaangalia sura wala wadhifa wa kiongozi, tunataka waachie nyumba ili watumishi wengine wapate fursa ya kuishi katika makazi bora," alifafanua.

Mayemba alisema mtu anayeweza kusamehewa kuhamishwa ni yule atakayelipa mapema kabla ya dalali wa mahakama kufika eneo la tukio. Atakayelipa wakati dalali wa mahakama anafanya kazi.

"Baada ya zoezi hili kufanyika, taratibu za kisheria zitachukuliwa kwa mtumishi aliyetumia mali ya umma bila kulipia. Zoezi hili linatarajia kuchukua zaidi ya wiki tatu.

"Tukitoka hapa tunakwenda Masaki, Chole, Mikocheni, Oysterbay, Ilala, Temeke na maeneo mengine yenye nyumba za serikali," alisema Mayemba.

Pia aliwakaribisha watu binafsi kuchangamkia fursa ya kupanga katika nyumba hizo. Akibainisha kuwa lipo eneo lingine Masaki ambako kunajengwa kwa ajili ya kutoa fursa kwa watumishi binafsi.

Alipoulizwa kuhusu gharama ya pango katika nyumba hizo, kiongozi huyo alisema nyumba zao zinatofautiana kutokana na eneo lakini kiwango cha kodi kilichowekwa ni rafiki kwa kukuwezesha mwananchi wa kawaida kumudu gharama.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma, wakibadilishana mawazo na wanufaika wa WCF, jijini Dar es Salaam jana. Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wenye Ulemavu yataadhimishwa Desemba 2 mwaka huu, jijini Dodoma yatakayolenga kukuza uelewa wa masuala ya ulemavu na kuhamasisha uungwaji mkono kwa ajili ya utu, haki na ustawi wa watu wenye ulemavu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## FCC yaandaa mafunzo kwa wafanyabiashara, wakulima

**Na Faustine Feliciane**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Ushindani Dunia Desemba 5 mwaka huu, Tume ya Ushindani (FCC) imepanga kuendesha mafunzo kwa makundi mbalimbali kufahamu uelewa wa shughuli za tume hiyo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana wakati wa uzinduzi rasmi wa Wiki ya Ushindani Duniani, Mkurugenzi Mkuu wa FCC, Dk. William Erio, alisema kuwa kuelekea kilele cha siku hiyo duniani, watatoa mafunzo kwa makundi mbalimbali kuhusu shughuli zinazofanywa na tume hii.

Aliyataja makundi hayo wataanza nayo ni ya wachimbaji madini mikoani Shinyanga na baadaye kufuatiwa na mafunzo ya sekta ya wazalishaji na wauzaji wa mbegu za maua kwa mikoa ya kaskazini; mafunzo yatafanyika mkoani Arusha.

"Pia tumelilenga kundi la wakamuaji zabibu na alizeti. Semina yao itafanyika jijini Dodoma," alisema Dk. Erio.

Alisema wataendelea na mafunzo hayo kwa kundi la wafanyabiashara na watu wa viwanda mkoani Mbeya kabla ya kumaliza mafunzo na wakulima wa korosho mkoani Mtwara.

"Tunataka watu hawa ambao kwa namna moja au nyingine wanazalisha bidhaa na kufanya biashara kufahamu shughuli za FCC na kuwa na ushirikiano zaidi wa kazi," alisema mkurugenzi huyo.

Poa alisema kwa mwaka huu kauli mbiu ya maadhimisho hayo ambayo kilele chake kitafanyika Dar es Salaam ni 'njama baina ya washindani na madhara yake kwa walaji'.

Alisema wanataka kuona kila mfanyabiashara anafuatana na kuzingatia kanuni za biashara. Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji anatarajiwa kuwa mgeni rasmi siku ya kilele cha maadhimisho hayo.

# 'Mifumo ya elimu iakisi mapinduzi ya viwanda'

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa elimu kutoka mataifa 11 wamesema kuna haja kuboresha mifumo ya elimu ili iakisi mapinduzi ya nne ya viwanda kwa kutoa wahitimu wenye uwezo mkubwa wa kufanya kazi.

Katika mkutano na waandishi wa habari wakati wa mkutano wa kimataifa wa kujadili ubora wa elimu, Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Ochola Wayoga, alisema jana kuwa wadau hao wanataka nchi za Afrika zisibaki nyuma kuwekeza zaidi kwenye mfumo wa elimu unaoakisi mapinduzi hayo ya viwanda.

Alisema wadau hao wanataka mfumo wa elimu ulenge zaidi kumwandaa mwanafunzi kuwa na ujuzi mkubwa wa kufanya kazi na kujiajiri.

"Mkutano huu una malengo makuu matatu; kufikiria na kujadili mchango wa sekta ya elimu katika mapinduzi ya viwanda na wanaona kwamba teknolojia inabadilika, hivyo hakuna haja ya kuendelea kuwa na mfumo wa elimu au kufundisha mifumo ileile isiyoakisi mapinduzi hayo ya viwanda.

"Na kama tutaendelea na mifumo hii, tutakuwa tunarudi nyuma. Kwahiyo, mwaka huu tutabainisha maeneo ya kuboresha kwa Tanzania, pia kwa nchi hizi zinazoshiriki mkutano huu.

"Na tunatoa rai serikali zetu za Afrika zinapotengeneza sera, kuandaa bajeti au kusimamia mifumo ya elimu. Kama nchi tusiachwe nyuma, vinginevyo tutatoa watu ambao hawawezi kufanya kazi au hawawezi kujiajiri."

# Wananchi 9,000 vijiji sita kunufaika mradi wa maji

**Na Steven William,** MUHEZA

WAKAZI 9,361 kutoka vijiji sita vya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, watanufaika na mradi wa majisafi na salama ambao unatekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani humu.

Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Muheza Tanga ikiongozwa na Katibu Tawala wilaya hiyo, Mohamed Mfaki, jana ilifika kukagua mabomba ya maji na mitaro katika vijiji cha Kwabastola na Makole.

Meneja wa RUWASA Wilaya ya Muheza, Juma Seleman alisema kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 na 2023 /24, mamlaka imetekeleza ujenzi wa mradi wa maji wa Mizembwe awamu ya pili unaohudumia vijiji sita.

Alivitaja vijiji hivyo ni Bwembwera, Msowelo, Miyanga, Makole, Mamboleo na Kimbo vyenye jumla ya wakazi 9,361.

Selemani alisema mradi huo unatekelezwa na mkandarasi M/D Dask Investment Company LTD kwa jumla ya gharama ya Sh. 2,529,858,826. Ulianza kutekelezwa Aprili mwaka huu na unatarajiwa kukamilika Aprili mwakani. Chanzo cha mradi huo ni Mto Malale.

Alisema mradi huo utakapokamilika utasaidia jamii katika upatikanaji maji safi na salama, hivyo kupunguza magonjwa yatokanayo na ukosefu wa maji safi na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Vijijini.

Katibu Tawala Wilaya ya Muheza Tanga, Mohamed Mfaki alimwagiza mkandarasi huyo kukamilisha mradi huo kwa wakati ili wananchi wanufaike na fedha nyingi zinazotolewa na serikali.

Msimamizi wa mradi huo kutoka kampuni ya M/S Dask Investment Company LTD, Rorgers Mahale alisema kazi waliyoifanya imefikia hatua nzuri huku akiahidi kukamilisha ujenzi kwa wakati na maelekezo aliyopewa na serikali ameyapokea, atayafanyia kazi.

# Canada, mashirika 35 kuteta kukuza usawa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI ya Canada kupitia ubalozi wake nchini, itakutana na mashirika 35 ya kiraia ya mikoa ya Kilimanjaro na Arusha ilikokuwa inatekeleza mradi wa kukuza usawa na elimu ya haki za binadamu (AEHRE).

Mradi huo wa miaka mitano unaohitimishwa rasmi siku hiyo, ulikuwa unatekelezwa na Shirika la TUSONGE CDO kwa ushirikiano na mashirika wenza chini ya ufadhili wa Kituo cha Kimataifa cha Elimu ya Haki za Binadamu (EQUITAS).

Jana Mkurugenzi wa Shirika la TUSONGE CDO, Agnatha Rutazaa, akizungumza katika warsha ya tathmini ya utekelezaji wa mradi huo, alisema watakaa kwa pamoja siku hiyo ili kutafakari nini kifanyike na kuona uendelevu wa kazi hiyo.

"Tunategemea kuwa na mashirika 35 yaliyoshiriki kwenye mradi huu, kutoka Arusha yako 17 na Kilimanjaro 18. Pia tunategemea kuwa na wanajamii walioshiriki kwenye kazi za jamii ambao ni watu 120.

"Katika tukio hili, tutazama kwa kina kuona nini tulichokifanya. Tutakaa pamoja siku hiyo na kutafakari nini kifanyike na hasa kuona uendelevu wa hii kazi unafanyikaje.

"Tutakubaliana kwamba tunakwenda kufanya nini kwa tulichokifanya kwa miaka mitano kibaki Tanzania, kifaidishe Watanzania wengi na mwisho wa siku tuweze kuona ukatili wa kingono unaisha kabisa," alisema.

Mshirika mwenza wa mradi huo, Gamaliel Mbalase, alisema moja ya mafanikio waliyoanza kuyaona kuanzia ngazi ya mitaa, kata na vitongoji katika Kata ya Bomambuzi, Manispaa ya Moshi, baada ya kuwajengea uwezo watoa uamuzi viongozi wa mila na dini, kumekuwa na ongezeko la uelewa katika masuala ya haki za binadamu.

"Pia tunaanza kuona wale viongozi wa dini wamebadilika kidogo na wanashiriki, lakini tuna viongozi wa kimila na wenyewe wameahidi baadhi ya vile visa asili kama mila zilizopitwa na muda watazifanyia kazi," alisema.

Tujanael Msuya ambaye ni mshiriki mwenza alieleza zaidi: "Tumeona wanawake wengi wanashiriki lakini si kushiriki kikamilifu na asitoe mawazo yake, wala maoni yake. Kwa hiyo, tulikuwa tunawajengea uwezo pamoja na watoto ili kushiriki kikamilifu ikiwezekana kuanzia ngazi ya familia, mitaa mpaka ngazi ya kata ili kuleta usawa katika ngazi ya maamuzi."

# RC aagiza kutungwa sheria ndogo wanaopitisha mifugo barabarani

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, ameziagiza halmashauri za mkoa huo kuboresha sheria ndogo ili kuwabana wafugaji wanaopitisha mifugo yao katika barabara na kuigharimu serikali kutumia fedha nyingi kufanya matengenezo.

Queen alitoa agizo hilo jana wakati wa kikao cha Bodi ya Barabara alipozungumza na wajumbe wa Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Manyara.

"Halmashauri nendeni mboreshe sheria ndogo na kuendelea kutoa elimu ya matumizi ya barabara ili tuokoe barabara zetu maana tunatumia fedha nyingi kuzifanyia matengenezo," alisema Sendiga.

Alisema wakurugenzi na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) wakianza kusimamia sheria ndogo na viongozi wa kisiasa wanyamaze wasiwatetee wafugaji.

"Wanasiasa tuache kupiga simu kwa mabosi wangu, niambieni mimi wakati mwingine mnanipa hofu," alisema.

Kuhusu ahadi za viongozi, Mkuu wa Mkoa aliagiza sekta zote zipeleke mpango kazi ofisini kwake kuonesha namna ya kwenda kutekeleza ahadi hizo.

"Ni lazima ahadi za viongozi zitekelezwe na madaraja makongwe ni vizuri kuyaangalia namna ya kuyatengeneza," alielekeza.

Awali Kaimu Meneja wa TANROADS mkoani Manyara, Dutu Masele, akiwasilisha taarifa yake, alisema wameishafanya uthamini kwa wananchi wanaotakiwa kulipwa fidia itakapopita barabara ya mchepuko ambapo Sh. bilioni tisa zitatolewa kuwalipa.

"Tumeishawasilisha wizarani ombi la kulipa fidia barabara ya mchepuko ya kilometa 25," alisema Masele.

Meneja huyo alitaja vikwazo ambavyo wanakabiliana navyo kuwa ni pamoja na mfumo wa ununuzi kuchelewa, mifugo kutembezwa barabarani, ufinyu wa bajeti na kutupa taka kwenye mitaro.

Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alisema kama hawatawapa kazi makandarasi wazawa hawatainuka kiuchumi badala yake makandarasi wa kigeni ndio wataendelea kunufaika.

Queen aliitaka TANROADS kuwashirikisha wabunge kwenye kazi wanazofanya kabla hawajaanza.

Kaimu Meneja wa TARURA Mkoa wa Manyara, Edwin Magiri, akitoa taarifa yake alisema utekelezaji miradi ya maendeleo umefikia asilimia 65 na mikataba 74 ya ujenzi wa barabara imeishatiwa saini.



Mwili wa Mtanzania Clemency Mtenga (22) aliyepoteza maisha kutokana na vita kati ya Israel na Hamas akiwa masomoni, ukipokelewa baada ya kuwasili nyumbani kwao Kijiji cha Kirwa, wilayani Rombo, mkoani Kilimanjaro kabla ya maziko juzi. **PICHA: MARY MOSHA**.

# Pinda apata mwarobaini uharibifu mazao sokoni

**Na Godfrey Mushi,** ARUMERU

MWENYEKITI wa Baraza la Taifa la kumshauri Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu masuala ya kilimo na lishe, Mizengo Pinda, amesema serikali na wabia wa maendeleo, wanapaswa kufikiri kuhusu uwekezaji vyumba vya baridi kwa ajili ya utunzaji mazao kwenye masoko ili kupunguza uharibifu wa mazao yanayopelekwa katika masoko na wakulima.

Amesema licha ya juhudi za serikali na wadau katika kuhamasisha masuala ya lishe, kuna tatizo kubwa la lishe nchini ambalo linasababisha madhara ikiwamo utapiamlo.

Kutokana na tatizo hilo, alisema ni wakati wa serikali za mitaa kulibeba suala hilo kama ajenda maalum kwa kuangalia namna ya kutoa elimu kwenye jamii katika ngazi mbalimbali ikiwamo kuwatumia maofisa maendeleo ya jamii.

Pinda, Waziri Mkuu mstaafu, aliyasema hayo jana alipozungumza na wadau wa kilimo katika maadhimisho ya miaka 50 ya Kituo cha Utafiti wa Mboga na Matunda cha Kimataifa (World Vegetable Center).

Alisema maofisa maendeleo ya jamii hawajatumika ipasavyo katika kubebeshwa mzigo huo wa kutoa elimu ya lishe na kuwa endapo watatumika vizuri watatoa elimu kwa jamii ikiwamo athari za magonjwa yasiyoambukiza yanayotokana na masuala ya mifumo ya chakula.

"Bado tuna tatizo kubwa nchini la lishe sasa, mimi si mtaalamu, lakini madhara yake tumeyaona.

"Nilikuwa nimeuliza kabla sijaja hapa kwani mikoa inayoongoza ni ipi? Wakaniambia Iringa, Njombe, Rukwa, ninakotoka.

"Wanasema hali ya utapiamlo ni kubwa na ninasema haya ili mwone umuhimu wa taasisi hii katika kujenga taifa lenye afya ambalo ndilo tunalolihitaji.

"Maofisa hawa wanaotoka kwenye vyuo vyetu tukiamua kuwasaidia watusaidie kuchangisha mawazo haya wana uwezo mkubwa sana.

"Watumieni kusaidia kueleza hili jambo kwa wananchi, mbona zamani walikuwa wanatufundisha tuchimbe vyoo, wakati mwingine tulikuwa tunajiuliza tuchimbe vyoo vya nini, lakini baadaye tukaelewa," alisema.

Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini wa kituo hicho, Dk. Gabriel Rugalema, alisema taasisi imeweza kuwekeza fedha nyingi kwa ajili ya kujenga benki bora ya vinasaba vya mbegu katika ukanda huo ambayo inajengwa kituoni huko. "Lengo ni kuhakikisha uzalishaji na utunzaji mbegu za asili za mboga za Kiafrika unaendelea pamoja na kufanya utafiti wa afya ya mimea ambao umesaidia katika kulinda mazao ya mboga dhidi ya wadudu na milipuko ya magonjwa, kupunguza upotevu wa mazao kutokana na wadudu na magonjwa kwa kutumia mbinu rafiki kwa mazingira," alisema.

"Tafiti hizi zimekuwa zinasaidia utimilifu wa uwezo katika sekta ya kilimo cha bustani, na kuongeza chakula, usalama wa lishe kwa mamilioni ya wakulima wadogo na watumiaji wa mboga," alisema Dk. Rugalema.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Emanuela Kaganda, alisema kuwapo taasisi hiyo katika Mkoa wa Arusha, umewajengea uwezo wakulima wadogo zaidi ya 1,000 na kuwezesha shule za msingi na sekondari zaidi ya 50, hivyo kufikia wanafunzi zaidi ya 5,000.

"Wakulima pamoja na wanafunzi wameweza kujifunza namna nzuri ya kushiriki kilimo cha mboga, hivyo kuboresha lishe wanayokula shuleni na katika kaya zao," alisema.





# Wafanyabiashara walia na TRA vishoka

**Na Thomas Slyvanus,** SAUT

BAADHI ya wafanyabiashara mkoani Mwanza wameiomba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani hapa kuingilia kati suala la watu wanaojifanya maofisa wa TRA maarufu kama 'Vishoka' ambao wamekuwa wakiwatapeli kwa njia ya simu na wengine kufika madukani wakihitaji kuwasaidia huduma mbalimbali ikiwamo kulipa kodi.

Wametoa ombi hilo kwa nyakati tofauti wakizungumza na Nipashe kufuatia kukithiri kwa watu hao ambao wakati mwingine wamekuwa wakifanikisha utolewaji wa huduma husika lakini kwa gharama tofauti na zinazotambulika kisheria.

"Tunaomba kwanza itolewe elimu kwetu juu ya namna ya kuwatambua ili kuepuka kutapeliwa kwani wamekuwa wakiturudisha nyuma katika biashara zetu."

"Kuna muda wanakuja kama watoa huduma kawaida na kusaidia katika upatikanaji leseni lakini kwa gharama zaidi na muda mwingine ukiwapa hela hawarudi tena," alisema Rahim Ramadhani mfanyabiashara ya nguo kutoka Igoma.

Mfanyabiashara mwingine kutoka Buzuruga, Sada John alisema vishoka wamewahi kufika katika kazi zake na kukagu wamweleza kuwa ana muda wa mwaka mmoja hajalipa kodi hivyo alitakiwa kulipia kodi pamoja na faini yake na kumtaka atoe fedha hiyo.

"Walichukua fedha yote niliyokuwa nayo wakinitishia pia kunifungulia mashtaka hali hiyo ilinifanya nifirisike kwa muda kutokana na kuishiwa mtaji niliokuwa nao," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa TRA Mkoa wa Mwanza, Moreri Mtui, aliambia Nipashe kuwa tatizo hilo wameanza kulifanyia kazi katika maeneo mbalimbali mkoani hapa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya mlipakodi na utambuzi wa maofisa TRA kwa wafanyabiashara.

"Jambo hili ni endelevu mkoani hapa na tayari tumefanya katika maeneo mbalimbali kama vile Kwimba, Buchosa na Usagara. Semina zilizotolewa ni kuhusu elimu ya kulipa kodi kwa wakati na matumizi ya mashine za kielektroniki pia kuwatambua maofisa wa TRA kwa kuwaomba kodi au kupiga simu ofisini kupata taarifa za maofisa hao," alisema Mtui

Pia aliwataka wafanyabiashara kujiridhisha kwa kuwaomba vitambulisho maofisa wanaowatembelea pia waache kulipa kodi kwa njia ya simu na badala yake watumie mawakala wa TRA walio karibu yao au kufika katika ofisi za TRA.

"Ukipigiwa simu na mtu kwamba utume kodi kwa njia ya simu tafadhali usifanye hivyo. Mteja analipa kodi kwa kujitengenezea 'control number' na kwenda kwa wakala au benki iliyo karibu yake," alisema Mtui.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, ACP Janeth Magomi, akionyesha kwa waandishi wa habari pikipiki 11 zilizokamatwa zikiwa zinamilikiwa na watu bila ya kuwa na nyaraka halali na kuhofiwa kutumika katika vitendo vya uhalifu, baada ya kutoa taarifa ya utendaji ya jeshi hilo kwa mwezi uliopita mkoani humo jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Gramu 2,000 dawa kulevya zakamatwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, limekamata vitu mbalimbali zikiwamo dawa za kulevya aina ya bangi gramu 2,205 na kete 61, mifuko 24 ya saruji, ndoo nne na makopo manne ya rangi inayotumika katika ujenzi wa nyuma za walioathriwa na tope la mgodi wa Mwadui.

Pia limekamata pikipiki 11 na 'gypsum powder' pamoja na vifaa mbalimbali vya ramli chonganishi vinavyotumiwa na waganga wa jadi wasio waadilifu vilivyopatikana kutokana na msako uliofanyika katika maeneo mbalimbali mkoani hapa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Janeth Magomi, alisema hayo jana wakati alitoa taarifa ya kukamatwa kwa vitu hivyo kwa vyombo vya habari.

Alisema jeshi hilo limekuwa likifanya doria za kuimarisha ulinzi na usalama na kushirikisha vikundi vya ulinzi shirikishi na hadi sasa vikundi hai 209 wanashirikiana navyo.

Kamanda Magomi alisema katika msako huo, watuhumiwa 29 walikamatwa huku baadhi yao wakifikishwa mahakamani na wengine kupewa dhamana wakisubiri upelelezi wa kesi kukamilika, hivyo kuwataka wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwa kuwa ni sehemu ya uvunjifu wa amani kwenye jamii.

Magomi pia alisema katika kipindi hicho, walikamatwa madereva 6,499 na kufikishwa mahakamani kwa makosa mbalimbali ya usalama barabarani, kati yao, watatu walifungiwa leseni zao na wengine kutozwa faini.

# Idadi kubwa wanafunzi sekondari usikivu hafifu hawajui kuandika

**Na Halima Ikunji,** TABORA

UTAFITI uliofanywa na Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu Mohayo (AMUCTA) mkoani Tabora kwa wanafunzi wa sekondari wenye usikivu hafifu, umebaini asilimia 59 ya wanafunzi hao hawajui kuandika na kusoma lugha za alama.

Kwa mujibu wa utafiti huo, hali hiyo inatokana na kutokuwa na msingi mzuri katika shule za msingi.

Ofisa Elimu Taaluma Mkoa wa Tabora, Aaron Vedasto, alisema hayo juzi katika warsha ya wadau wa sekta ya elimu kwamba katika utafiti huo, walibaini wanafunzi 404 kuwa na tatizo hilo huku kati yao 96 wakiwa hawawezi kabisa kuandika na 86 wana uwezo wa chini wa kuandika na kuongea lugha ya alama.

Alisema hali hiyo inaibua changamoto kwenye mikakati ya serikali katika sekta ya elimu jumuishi unaolenga kuwaweka pamoja wananfunzi wenye mahitaji maalum ili kuleta usawa na kuondoa unyanyapaa wengi wao waliachwa nyuma.

"Nakiri bado tatizo ni kubwa kwenye elimu jumuishi lakini serikali itaendelea kupokea maoni na kuyafanyia kazi na kuona namna gani itaweza kufanya maboresho katika sekta hii muhimu hapa nchini," alisema Vedasto.

Akisoma taarifa ya utafiti katika kikao cha kitaaluma, Padri Dk. Apolinary Ndasi kutoka AMUCTA alisema wajibu wao ni kufundisha, kufanya utafiti na kutoa huduma kwa jamii.

Dk. Ndasi alisema chuo hicho kiliweka mikakati baada ya kuona mianya inayojitokeza kwenye elimu ya wanafunzi wasiosikia wengine kuacha shule na uzoefu wa walimu katika ufundisha kuwa ni tatizo kubwa.

"Tulipoona tatizo tulitoa maarifa na kuwaweka walimu wenye ujuzi ambao wataweza wafundisha wanafunzi hao kupunguza ama kumaliza kabisa tatizo hilo kwa watoto wetu," alisema Padri Dk. Ndasi.

Pia alisema chuo hicho kililenga kuwaendeleza walimu wakuu na waratibu elimu kata kuwaongezea ujuzi na usimamizi wa uwendeshaji katika shule za wanafunzi wenye usikivu hafifu.

Ofisa Elimu Kata ya Mwinyi mkoani hapa, Mwalimu Masumbuko Abeli, aliwashauri maofisa elimu wote kufanya upembuzi yakinifu kwa walimu wa kufundisha wanafunzi wenye uhitaji maalum kama wana ustadi katika ufundishaji.

Mthibiti Ubora Mkuu wa Shule za Manispaa ya Tabora, Florencia Vincent, aliishukuru serikali kwa kuwaletea walimu vifaa mbalimbali na kuomba iendelee kuongeza walimu wenye ujuzi wa elimu na taaluma kwa kuwa kwa sasa hawatoshi kutokana na idadi ya wanafunzi iliyopo.

**ama**
ALHAMISI NOVEMBA 30, 2023
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

## VITA MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA... Kisukari namna ya kukimudu ni mtihani



## Hatari kansa kwa wanafunzi kula vyakula, vifungashio vya plastiki

Ukurasa 13

VITA VYA MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA…

# Kazi ya Rais tangu kuzindua bungeni, hadi mwendelezo anaodumisha sasa

**Na Mwandishi Wetu**

ILIKUWA mapema mwaka 2021, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akatangaza kuanza kazi kwa serikali yake ya awamu ya sita, ikiweka nguvu kuendeleza kazi ya tiba ikiwamo kwa magonjwa yasiyoambukiza kusababisha vifo vingi, pia zikiigharimu serikali fedha nyingi.

Hiyo ilikuwa mnamo Aprili, kwenye kikao cha Bunge jijini Dodoma, katika hotuba yake ya kwanza akiwa rais.

Mara moja, Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza (TANCDA), likaguswa na kumtumia pongezi Rais Dk. Samia, serikali yake kuweka vipaumbele vya serikali yake vita dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza au 'NCD'.

Hapo TANCDA wakafafanua kilichowagusa, mkuu wa nchi kutambua madhila yanayowapata wagonjwa wengi na kuahidi kuimarisha mifuko ya bima ya afya ziwafikie Watanzania wote, jambo ambalo limekuwa ni kilio cha shirikisho hilo kwa muda mrefu.

Ufafanuzi huo wa rais, una azma ya serikali kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa na kuzipeleka kwenye hospitali za rufani kwa mikoa yote nchini.

Ahadi ya Rais Dk. Samia kwa umma, ikawa serikali ingeimarisha utoaji huduma za matibabu kwa wazee na kuweka mipango maalum kuhudumia makundi yenye magonjwa adimu.




Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu. **PICHA: MTANDAO**

Hapo ndipo akatambulisha namna serikali yake ingeimarisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, ili kufikia lengo la 'Bima ya Afya kwa Wote' akitoa takwimu kwa wakati huo ni watu 8,224,271 sawa na asilimia 14 tu ya Watanzania, ndio waliotumia bima ya afya.

"TANCDA imefarijika sana na mkakati huu wa serikali Awamu ya Sita, kwa kuzingatia kwamba magonjwa haya yasiyoambukiza yanaongezeka kwa kasi na hata kuwaathiri watu wenye umri mdogo, wakiwamo watoto.

"Tafiti za kisayansi zinaonyesha kuwa mwaka 2016, watu milioni 42, sawa na asilimia 71 ya vifo vyote duniani walipoteza maisha kutokana na magonjwa yasiyoambukiza.

Pia, asilimia 75 ya vifo vyote vinavyohusu watu wenye umri kati ya miaka 30 hadi 70," inatamka taarifa ya wadau.

Nchini Tanzania kunakadiriwa magonjwa haya yanasababisha asilimia 27 ya vifo vyote na utafiti wa mwaka 2012, unaonyesha kwa kila watu 100 wenye mri kuanzia miaka 25 na zaidi, tisa wanaugua kisukari; 26 wana shinikizo la damu; 25 mafuta yaliyozidi kwenye damu; na 34 uzito ulizidi.

"Tunatambua wazi kuwa juhudi hizi za Mama Samia, amekuwa akizitekeleza tangu akiwa Makamu wa Rais katika Serikali ya Awamu ya Tano. Mwaka 2016, alihamasisha wananchi kufanya mazoezi ya mara kwa mara ili kukabiliana na magonjwa haya yasiyoambukiza.

"Kwa kutambua kwamba magonjwa haya yasiyoambukiza ni janga linaloandama jamii, alitangaza kila Jumamosi ya pili ya mwezi iwe siku ya kitaifa ya mazoezi.

"Mara kadhaa kwa nyakati tofauti alikuwa akionyesha kwa vitendo ufanyaji mazoezi," akatamka aliyekuwa Katibu wa TANCDA, Prof. Kaushik Ramaiya, akiambatanisha na ahadi ya ushirikiano wao kupatikana.

**UTEKELEZAJI SERIKALINI**

Ndani ya kipindi hicho baada ya tangazo la Rais Dk. Samia, Wizara ya Afya yenye dhamana husika, ikataja hatua kuanza na ikaorodhesha magonjwa yasiyoambukiza kama saratani, kisukari na shinikizo la damu yanachangia kwa kiasi kikubwa vifo vya watu hospitalini.

Kupitia taarifa yake, Prof. Abel N. Makubi, aliyekuwa Katibu Mkuu wa wizara hiyo, ni kwamba magonjwa hayo yasiyoambukiza yanachangia wastani wa asilimia 40 hadi 45 za vifo wakati huo, ikilinganishwa na asilimia 33 miaka mitano kabla, yaani mwaka 2018.

Taarifa ikakumbusha hatua za kuchukuliwa kujihami, ikiwamo shuleni na kwenye familia kutoa fursa ya kujikinga mapema kwa kutumia vigezo kama "kufanya mazoezi, kupunguza vyakula vya mafuta, pombe, chumvi nyingi, kuepuka unene na kuacha kuvuta sigara."

Ni zama ambazo maradhi ya Ukimwi na malaria, yakitajwa kupungua kwa zaidi ya asilimia 60, kati ya mwaka 2015 na 2020. Wizara ya Afya, hapo ikasisitiza haja yya kujihami kwamba:

"Tahadhari iliyotolewa hivi karibuni (April, 2021) na Rais wetu Samia Suluhu Hassan, kuwa Watanzania waendelee kuchukua tahadhari za kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Covid -19..."

**WIZARA AFYA 2023**

Miaka miwili baadaye, mnamo Julai 2023, Wizara ya Afya, ikafafanua kwamba magonjwa yasiyoambukiza yanachangia takribani 33 ya vifo vyote nchini, huku

Inaendelea Uk. 12

AFYA

## VITA VYA MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA…

# Kisukari namna ya kukimudu ni mtihani

Na Romana Mallya

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), linasema ugonjwa wa kisukari ndio chanzo kikuu cha upofu, figo kushindwa kufanya kazi, mshtuko wa moyo, kiharusi na watu kukatwa viungo vya chini vya miguu.

Mwaka 2016 kumekadiriwa vifo milioni 1.6 vilivyotokana na kisukari, huku Shirikisho la Kimataifa la Kisukari linakadiria asilimia 80 ya watu wazima wanaoishi na hali hiyo wako katika nchi za kipato cha kati na chini, tabia yao ya ulaji ikibadilika kwa kasi.

Wataalamu wa Afya Tanzania, wanaeleza shaka yao kuwa watu wengi kutumbukia katika hatari ya changamoto tajwa, endapo hawatabadili mwenendo wa maisha yao.

Ni undani unaoibuliwa kwenye mkutano wa siku moja jijini Dar es Salaam, ulioandaliwa na Chama cha Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA), kuhusu kisukari na changamoto zake, ukikutanisha wataalamu wa afya na wagonjwa wa kisukari.

Daktari kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Joachim Kilemile, anasema kisukari kina athari katika pazia la kuona (retina), ilibaki tatizo kubwa hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara.

"Inatarajiwa wagonjwa watakuwa mara mbili zaidi ifikapo 2035, kutoka milioni 21.5 hadi milioni 41.5, anatamka na kuongeza: "Upotezaji uono kutokana na kisukari unatarajiwa kuongezeka. Hadi sasa kiwango cha kuathirika kwa pazia kwa wagonjwa wenye kisukari ni asilimia 27.9."

Dk. Kilemile anataja vitu vinavyoweza kurekebishwa ni udhibiti wa sukari, shinikizo la damu (BP), kiwango cha mafuta mwilini, kubadili mtindo wa maisha na kuongeza kiwango cha mazoezi.

Pia anafafanua kisukari na magonjwa yanayotokana na kisukari yanaongezeka duniani kote, nchi za dunia ya tatu zikiathirika zaidi, sasa iko katika orodha ya magonjwa 10 yanayochangia vifo zaidi duniani na magonjwa mengine yasiyoambukiza.



Kampeni dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza ikiendelea. **PICHA: MTANDAO**

Anasema, madhara yake yameongezeka maradufu, waathirika wakubwa ni kundi la wenye umri miaka 20 mpaka 65.

### CHAMA CHA KISUKARI

Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Wanaoishi na Kisukari Aina ya Kwanza Tanzania (YDYA), Dk. Aniceth Muchunguzi, anasimulia ameishi na kisukari aina ya kwanza tangu mwaka 2013.

Anasema, kipindi alipogundulika kuwa na tatizo hilo, ilikuwapo tatizo kubwa la jamii kutofahamu ama vijana au mtoto anaweza kupata kisukari aina ya kwanza, hali iliyosababisha watoto na vijana wenye kisukari hicho kupoteza maisha kabla ya kugundulika.

Dk. Muchunguzi, anaisisitiza jamii, pale kasoro inapogundulika mapema, inamwezesha mtu kutimiza ndoto zake, akirejea mfano binafsi sasa ni daktari wa tiba.

Anafafanua kitaalamu, kisukari aina ya kwanza hutokea kinga ya mwili inaposhambulia kongosho na kushindwa kufanya kazi, akinena: "Inashindwa kutengeneza kichocheo kinachoitwa 'insulin' ambayo ndiyo hudhibiti kiwango cha sukari na kusababisha mtu kupata kisukari cha aina ya kwanza.

"Matibabu yake ni kutumia insulini bandia kila siku kudhibiti. Endapo mtu anamwona mtoto wake anapungua uzito haraka ndani ya muda mfupi, anakunywa maji sana na kuwa na kiu kilichopitiliza, licha ya kunywa maji, lakini hatosheki...

"Anakwenda haja ndogo mara kwa mara na usiku anaamka hadi mara nne, kuchoka, haoni vizuri au kichefuchefu ni vyema ampeleke hospitalini kuangalia kama ana tatizo hilo."

### AINA YA KISUKARI

Daktari huyo, anataja takwimu za dunia, zaidi ya watu milioni 500 mpaka 600 wana kisukari na kati yao, takribani milioni 10 wana kisukari aina ya kwanza.

Anasema, watoto wamekuwa hawagunduliki mapema, hivyo chama chao kimejikita kutoa elimu kwa jamii ibadilike na kwa shida hiyo ya kisukari, wanachohitaji zaidi ni kusaidiwa vifaa tiba, kwa kuwa insulini wanayoitumia kila siku ni ya gharama kubwa.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, mtu anaweza kutumia gharama mpaka shilingi milioni tatu kwa mwaka, kufikia matibabu sahihi ya kisukari cha kwanza.

Dk. Muchunguzi anaiomba serikali, iingilie kati suala hilo, kwa kuhakikisha matibabu yanapatikana kwa gharama nafuu au bure, ili kuhakikisha afya za wagonjwa waliopo.

Mtaalamu wa ugonjwa kisukari wa Hospitali ya Rufani Temeke, Dk. Boniface Mphumuhila, anasema mgonjwa wa sukari hadi kufikia kupata kidonda na kukatwa mguu, hutokana na kushindwa kudhibiti hali yake.

Dk. Mphumuhila anafafanua, sukari inapokuwa juu kwa muda mrefu, inaathiri mishipa ya fahamu na damu kutofanya kazi vizuri.

Anasema takwimu za Tanzania, zinaonyesha kila wagonjwa 100 wa sukari, kuna uwezekano wagonjwa watano mpaka 10 wanapoteza miguu kwa mwaka.

"Hivyo, wanawashauri watu wavae viatu vinavyoweza kuwafaa kwa afya na wenye shughuli zinazohusiana na moto kujiepusha na ajali za moto," anaeleza.

### KISUKARI NA FIGO

Daktari Bingwa wa Magongwa ya Figo Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Onesmo Kisanga, pia Rais wa Chama cha Wataalamu wa Figo Tanzania, anasema ugonjwa kisukari unaoongoza duniani kuchangia shida ya figo.

Anasema, utafiti nchini unaonyesha asilimia 44 ya kisukari kinasababisha shida ya figo na kuna wagonjwa waliosaidiwa kupandikizwa na kufanyiwa kusafisha damu.

"Muhimu ni kuzuia, kwa kuwa ugonjwa huu una hatua tano. Hatua ya kwanza na ya pili ni mapema, tunaweza kudhibiti magonjwa ya figo. Mtu akifika hatua ya nne na tano, tunafika kwenye kusafisha damu au upandikizaji wa figo, ambao ni ghali.

"Tunaposema mtindo wa maisha ndio lengo kuu, kupima mara kwa mara afya na vipimo vyenyewe si ghali. Ni kupima kisukari chenyewe, uzito na mkojo.

"Tunatoa elimu watu wapime angalau mara moja kwa mwaka na wasitumie dawa ovyo za kutuliza maumivu mfano...chakula kula kuzidi nayo inaleta tatizo," anasema.

Dk. Kisanga anasema wanaosafisha damu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, wapo vijana, ikimaanisha kwa umri wao hawakuweza kuzuia tatizo mapema.

"Kila siku wagonjwa wanaosafishwa damu Hospitali ya Muhimbili ni 200, wanaofika kila siku kwa ajili ya kuingia chumba cha upasuaji ni kati ya 40 na 50, wanaolazwa kwa magonjwa sugu ya figo ni zaidi ya 20 na wagonjwa mpaka 10 kwa magonjwa ya ghafla na ICU ni wengi," anasema.

## KAZI YA RAIS TANGU KUZINDUA BUNGENI, HADI MWENDELEZO ANAODUMISHA SASA

Inatoka Uk. 11

takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa mwaka 2020, zinaonyesha magonjwa hayo yalichangia zaidi ya vifo milioni 41 sawa na asilimia 71 ya vifo vyote duniani, ikilinganishwa na vifo milioni 57 duniani mwaka 2016.

Waziri wa Afya wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Nassor Mazrui, ana ufafanuzi wake alioutoa kwenye uzinduzi wa Utafiti wa Kitaifa wa Viashiria vya Magonjwa Yasiyoambukiza (steps survey 2023) uliofanyika jijini Dodoma.

Waziri Mazrui anaeleza, takwimu zinaonyesha magonjwa hayo yameongezeka mara tisa zaidi, akirejea miaka ya 80 ilikuwa asilimia moja tu ya Watanzania waliugua kisukari na asilimia tano, walikuwa na shinikizo la juu la damu.

Anasema kwa sasa, tatizo la kisukari limefikia asilimia tisa na shinikizo la juu la damu limeongezeka kufikia asilimia 25. Nako ana ufafanuzi:

"Takwimu hizo zote kutoka katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya nchini, zinaonyesha ongezeko kubwa sana la magonjwa hayo, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023."

Waziri huyo anaianisha magonjwa yaliyosababisha wagonjwa wengi kuhudhuria vituo vya huduma za afya, sasa, ni pamoja na shinikizo la juu la damu, 1,456,881 sawa na asilimia 49, ikilinganishwa na asilimia 34 kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/2022.

Pia anataja kisukari kuchangia wagonjwa 713,057 sawa na asilimia 24, magonjwa ya mfumo wa hewa 386,018 sawa na asilimia 13, ikilinganishwa na asilimia 10 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/2022.

Anasema katika kukabiliana na ongezeko la magonjwa hayo, hatua za kiserikali katika uongozi wa Rais Dk. Samia, zinajumuisha mkakati wa kitaifa kukabiliana na magonjwa hayo, wakiielimisha jamii namna bora ya kujikinga.

Mengine anayataja ni kuimarisha mifumo ya utoaji huduma za afya nchini, ikianzia uchunguzi wa awali na matibabu kuanzia ngazi ya afya ya msingi.

Ni hoja inayosisitizwa na Rais Dk. Samia alipokuwa ziarani mkoa wa Mtwara, Septemba mwaka huu akiorodhesha majukumu ya msingi ya watumishi wa afya ni kuokoa maisha ya walengwa, wakijituma kwenye miundombinu, vifaa na dawa ambazo serikali imewekeza.

AFYA

# Hatari kansa kwa wanafunzi kula vyakula, vifungashio vya plastiki

## •'Aisikirimu', karanga, mihogo... wadai ina ladha
## • Madaktari bingwa na angalizo la balaa la afya

**Na Jenifer Gilla**

KWA sasa ni jambo la kawaida kukuta wafanyabiashara wamepanga bidhaa pembeni mwa shule za msingi na sekondari, wakiwauzia wanafunzi vitu vidogo vya kula kupooza njaa zao.

Baadhi ya vyakula vinavyopendwa na wanafunzi ni 'aisikirimu', karanga, ubuyu na tambi zinazouzwa zimefungwa kwenye mifuko laini ya plastiki wanauziwa watoto hao.

Vipo vyakula hupikwa hapo hapo na mwanafunzi anapoenda kununua, hufungiwa katika mifuko hiyo akitafuta nafasi jirani kujisitiri kwa mlo huo.

Uchunguzi wa Nipashe katika shule za serikali katika wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke mkoani Dar es Salaam, umegundua asilimia kubwa ya wanafunzi wanunuzi wa milo katika mifuko hiyo, wamekuwa wakitafuna mifuko na vyakula, hali inayohatarisha afya zao.

Katika Shule ya Msingi Tabata JICA, mwandishi wa gazeti hili akakikuta kikundi cha wanafunzi wanne waliokuwa wakila mihogo pamoja na mifuko hiyo, badala ya kuchukua kwa mkono na kutumbukiza mdomoni.

Anapoulizwa sababu ya kufanya hivyo, mwanafunzi mvulana anayejitambulisha kwa jina (tunalo) akasema anapokula kwa kutafuna mfuko, ladha inakuwa nzuri zaidi tofauti na kuchukua kwa mkono.

"Sio kwamba nameza mfuko, hapa ninapokuwa natafuna ninameza mihogo, mfuko unabaki mwisho kisha ninautema na kutupa, ingawa na wenyewe unakuwa umelainika sana," akanena.

Katika kituo cha mabasi cha Mtaa wa Uhuru, Kariakoo, mwandishi akashuhudia wanafunzi wawili wakinunua karanga, mmoja akatumbukiza mfuko wenye karanga mdomoni na kuanza kukitafuna.

Nipashe inapopotaka kufahamu sababu ya wanafunzi kufanya hivyo, mfanyabiashara wa bidhaa, Jamila Kassim, akamjibu "wanafunzi wamekuwa wakifanya hivyo kupata ladha nzuri mdomoni."

Muuzaji huyo akawatetea kwamba wanafunzi wanapokula mifuko hiyo inasaidia kuhifadhi mazingira, kwa sababu wanapokula karanga peke yake, wanatupa mifuko hiyo ovyo na kusababisha wao kusumbuliwa kufanya usafi.

"Mimi naona sawa tu, kwa sababu hawa watoto hawana ustaarabu na mazingira. Utakuta eneo zima limejaa vifuko vya karanga, huku sisi wauzaji tunaambiwa tuokote. Bora waitafune wakaiteme mbele huko, ikiwa imeshasagika," anasema.

Mwandishi alipomhoji muuzaji 'askirimu' kama haoni madhara kiafya kwa watoto kula mifuko ya plastiki, eneo la Mwenge, Dar es Salaam, akajibu mifuko hiyo haina madhara, kwa kuwa watu wamekuwa wakiila tangu zamani na hakuna aliyethibitika kupata tatizo kiafya.

Anaeleza uzoefu wake amekuwa akiuza bidhaa hiyo anakoishi muda mrefu, anawashuhudia watoto wa mtaani kwake wakila mifuko hiyo na hakuna madhara yoyote kiafya wanayopata.

"Ni suala la imani tu, mimi mwenyewe wakati nakuwa nimekula sana hii mifuko na ile yenye karanga na ubuyu na hakuna madhara niliyopata. Kwa sababu unaitafuna tu kama 'bigijii' halafu unatema," anasema.



Wanafunzi wakila vyakula vyenye vifungashio vya plastiki. **PICHA: JENIFER GILLA**

**MADAKTARI WAZUNGUMZA**

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Saratani kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dk. Emmanuel Lugina, anasema mtoto hata mtu mzima anayetafuna mifuko ya plastiki anajiweka katika hatari ya kupata ugonjwa wa saratani.

Anasema mtu huyo anapotafuna mifuko hiyo na akaisaga na meno kufikia chembe ndogo za plastiki zisizozidi kipenyo cha milimita tano, kisha akameza anaweza kupata ugonjwa huo kwa kuwa zinaaminika kuwa na kemikali za zebaki na Bisphenol A (BPA) kwa wingi, zinazosababisha mtu kupata saratani.

Dk. Lugina anasema, kemikali zebaki huleta madhara kama vile mtu kuzaa watoto wenye utindio wa ubongo, midomo ya sungura, kudhoofika mwili, kutetemeka na kupoteza kumbukumbu. Inatajwa kuvuruga mfumo wa ubongo na kusababisha kudumaa viungo vya mwili na ubongo.

Kuhusu kemikali ya BPA, anaeleza zinatajwa kuhusika na mabadiliko ya 'tishu'mwilini kuharibiwa kwa vina saba, mimba kuharibika, matatizo wakati wa uzazi na mabadiliko ya homoni.

"Haijulikani kama chembe chembe hizi peke yake au pamoja na uwapo kemikali kama zebaki na BPA katika hizi chembe chembe, ndio kisababishi cha ongezeko la saratani," anafafanua Dk.Lugina.

Pia anasema mtu anapomeza vipande vikubwa vya plastiki, anaweza kupata madhara kukwaruza au kutoboa utumbo na kupata maumivu ya tumbo iwapo kipande alichomeza kina ncha kali.

Anataja vipande vikubwa vinasababisha utumbo kufungamana na mtoto kushindwa kupata choo, anatapika, kuumwa tumbo na ikitokea imechafuliwa na kemikali zenye sumu kama vile zebaki, klorini na BPA, zina madhara pia kiafya.

"Ulaji wa plastiki kubwa ni jambo la nadra sana, basi hata kupata sumu hizo kwa kiwango kikubwa kupitia ulaji wa plastiki ni mdogo sana," anafafanua.

Daktari Bingwa wa Tiba ya Familia kutoka Hospitali ya Agakhan, Willbroad Kyejo, anasema ulaji mifuko ya plastiki inaweza kusababisha magonjwa ya kuharisha na kutapika, hata kipindupindu ikiwa utayarishaji wa bidhaa hiyo haukuzingatia usafi.

Anatahadharisha uandaaji bidhaa uzipozingatia usafi, unaweza kusababisha maambukizi ya bakteria, mtoto anapotumbukiza mdomoni na ikatokea kinga yake ya mwili ipo chini, anaweza pata magonjwa ya mlipuko.

Dk. Kyejo anashauri elimu ya madhara ya ulaji plastiki izidi kutolewe kwa wazazi na shuleni, ili hatua zichukuliwe na wadau hao wawili kuhakikisha watoto hawali bidhaa hizo.

Aidha, anashauri wafanyabiashara wa bidhaa za watoto zinazofungwa katika mifuko, kubadilisha vifungashio kuwapo zisizo na madhara kwa watoto na kuepusha ulaji mifuko ya plastiki.

Ni ushauri unaoedana na kuhimizwa matumizi mifuko plastikio kutafutiwa mbadala, kama inavyotumika kwenye 'aisikirimu' aina ya 'koni'.

Mnamo Aprili 9 mwaka 2019, serikali ilitangaza kupiga mafuruku kutengeneza, kuingiza, kuuza na kutumia mifuko ya plastiki kwa ajili ya kubebea bidhaa na matumizi yake yake ifikapo Mei 31, 2019, ikitaja vipimo maalum sheria inayokataza.

Pia Aprili 2021, Kurugenzi ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, ikatamka mafanikio ya marufuku ya utumiaji mifuko ya plastiki, yamekwazwa na changamoto ya matumizi ya vifungashio vya plastiki ambazo havikidhi viwango.

Aprili mwaka huu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, akatoa siku 30 kwa mameneja wa kanda zote za Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuendesha kampeni za kuondosha mifuko ya plastiki batili kisheria, inayochangia ongezeko la uchafuzi wa mazingira, hususan mijini.

MAZINGIRA

## KUKOMESHAJI UKATILI WA KIJINSIA

# Safari kudhibiti ukeketaji inaneemeka, wanaoipinga wakibaki 'mfupa mgumu'

## •Wabuni mbinu mpya kuvizia vichanga

**Na Zanura Mollel**

HADI sasa kunatajwa bado kuna ukatili dhidi ya maisha ya watoto, kinamama na vichanga, huku upande wa pili kitaifa kuna vita kukabili mila ukeketaji, tendo linalohusu kuondoa kiungo cha 'faragha' kwa binadamu wa kike.

Ni hali inayochukua nafasi, njama na matendo dhidi ya hatua za kiserikali nazo zinaendelea kwa ukeketaji kudumishwa kwa siri kubwa katika baadhi ya jamii nchini.

Kimsingi, ukeketaji umegawanyika katika staili nne, huku kukitendeka kwa namna ya kushona sehemu hizo katika mfumo wenye madhara maradufu kwa mhusika ikiambatana na matumizi ya kemikali kama jiki ukeni.



Kinamama waliokusanyika kupata elimu ya madhara ya ukeketaji. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### NGARIBA MSTAAFU

Kwa mujibu wa Ngariba Mstaafu (jina tunalo) wa jamii ya Kimasai, hofu iliyoko ni wakeketaji wanakwepa mikono ya serikali, sasa wanabadili mbinu wakiwakeketa watoto wachanga.

"Kabla sijaacha kazi ya ungariba, niliwahi kumkeketa mtoto mchanga kwa kutumia kucha. Mtoto yule alitokwa na damu nyingi sana akafariki, kwa sasa sifanyi shughuli hiyo, ila kuna wenzangu bado wanaendelea na kazi ya kukeketa," anatamka ngariba huyo.

### WADAU WA MASHIRIKA

Mkurugenzi Mtendaji Shirika la Health Intergrated Multisectoral Development (HIMD), Mackrine Rumanyika, anafafanua kuwa utafiti uliotolewa unaonyesha kupungua vitendo vya ukeketaji, lakini wanapoenda shuleni kuelimisha, wanagundua mengine ya siri.

Anasema, hilo hujitokeza wanapofunza aina za ukeketaji kwa kutumia picha za midoli, wanabaini watoto wengi wamefanyiwa kitendo hicho.

"Tunawapatia karatasi na kuwaambia kila mmoja aandike yeye ni namba ngapi kati ya midoli minne tuliyowaonyesha na tunawaambia wasiandike majina yao. Kupitia hili, tumebaini kweli watoto wanakeketwa wadogo," anasema Rumanyika.

Anatamka ni hali inayochangia kukosekana takwimu sahihi, huku hofu nyingine iliyopo kwa njia mbadala ya ukaguzi kliniki kwa 'vichanga' nayo inahatarisha idadi ya mahudhurio, ikizidishia shida jamii ya watoto kukosa huduma stahiki za afya.

### HALI KITAIFA

Mikoa ya Mara, Kagera na Dodoma, hadi sasa inatajwa kuwa kinara wa matukio ya ukatili, ikiwamo vipigo, mauaji na ubakaji.

Ni taarifa katika uzinduzi wa Kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), pamoja na Mtandao wa Kupambana na Ukatili wa Kijinsia (MKUKI), uliofanyika mkoani Dar es Salaam, wiki iliyopita.

Mwenyekiti wa WiLDAF, Dk. Monica Mhoja, anasema asilimia 40 ya vitendo vya ukatili, inafanywa kwenye mikoa hiyo, sababu kuu ni kukumbatia mila na utamaduni kandamizi.

"Tumefanya utafiti (mkoa)Mara, ndoa za utotoni bado zipo nyingi, mtoto miaka 14 analazimishwa kuolewa kwa baba mtu mzima," anatamka Mwenyekiti Monica.

Anaendelea: "Watoto wanapigwa mpaka kupasuliwa vichwa, wanazalishwa wakiwa na umri mdogo, wengi hupoteza maisha."

Mbali na kasoro hizo, Tanzania inatajwa kuwa miongoni mwa nchi zilizopiga hatua katika kupunguza ukeketaji kwa asilimia 75 na kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vilivyowekwa, nchini sasa ni asilimia 15.

Mwezi uliopita, Kamishna wa Afya, Haki za Binadamu na Maendeleo ya Jamii (HHS) wa Umoja wa Afrika, Balozi Minate Samate, katika Mkutano wa Kimataifa wa kutokomeza ukeketaji chini ya nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU), akitamka "Kenya ina kiwango cha wastani ikiwa na asilimia 27, wakati Uganda ina kiwango cha chini ikiwa na asilimia moja."



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima, akizungumza jambo na hadhira (haipo pichani) kuhusu athari za ukeketaji.

Mataifa ya Somalia, Guinea, Djibouti na Ethiopia, yanatajwa kuwa na kiwango kikubwa cha ukeketaji zikiwa na asilimia 98, kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa za mwaka 2022.

Inaelezwa kwamba, wasichana wenye umri wa miaka 15 hadi 49 wamekeketwa na asilimia 35 wamekeketwa wakiwa hawajafika umri wa mwaka mmoja.

Takwimu hizo zinaeleza wastani, katika wanawake 10 basi mmoja amekeketwa, huku akizitahadharisha nchi zenye viwango vya chini kuwa, utafiti unaonyesha jamii zinavuka mipaka kwenda nchi jirani kufanya ukeketaji, hivyo serikali zinapaswa kushirikiana kukomesha vitendo hivyo.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, anasema kati ya watu milioni 200 waliokeketwa duniani, nusu wanatoka nchi za Afrika na asilimia 20 wamekeketwa na wahudumu wa afya.

"Lazima tuseme imetosha ili kulinda wanawake milioni 68 walio katika hatari ya kukeketwa," anatamka Wazii Gwajima.

### MDAU NDOA UTOTONI

Mkurugenzi wa Shirika la Mimute Women Organization (MWO), Rose Njilo, anasema ndoa za utotoni na za lazima bado kinara kwenye jamii za kifugaji na shirika limefanikiwa kuokoa watoto 17 kutoka wilaya za Longido, Monduli na Ngorongoro.

"Mabinti hawa tumewaokoa ambao tayari walikuwa wameshapelekwa kwa waume baada ya kutolewa shule na wengine tuliwawahi kabla hajapelekwa kwa mume. Hali ni tete bado kwa jamii ya Kimasai," anatamka.

Anasema, wamefanikiwa kushinda kesi mbili ambazo zilihusisha 'vitendo vichafu' vikihusisha watoto wenye umri miaka saba na mitano na watuhumiwa wamehukumiwa vifungo vikubwa, wilayani Ngorongoro.

### MTAFITI HAKI ZA BINADAMU

Mtafiti wa Haki za Binadamu, Asasi ya Center for Human Rights University of Pretoria, Halima Sonda, anataja chanzo mojawapo ni uhamaji usio rasmi na usafirishaji haramu wa binadamu; wanawake na watoto, wamekuwa wakipokea matukio ya kikatili.

Halima anasema kundi hilo limekuwa likipitia madhila ya ubakaji, ulawiti na vipigo kupitia mtandao wa wasafirishaji, ukatili na watoto wakitumikishwa kazi na biashara ya ngono.

"Tanzania kumekuwapo na usafirishaji wa ndani ambao watoto hususani mabinti, hutolewa vijijini na kuletwa miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha na Zanzibar wakidanganywa kuja kufanya kazi.

"Ila wanapofika, hutumikishwa katika biashara ya ngono, wengine wanapitia vipigo na kunyimwa chakula," anaeleza Halima.

### RIPOTI UN-WOMEN

Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya UN Women, chombo cha Umoja wa Mataifa kinachoshughulikia Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji Wanawake, Sarah Hendriks anasema takwimu zinaonyesha dunia inashindwa kusonga mbele, kufikia usawa wa kijinsia, hata kugeuka kuwa lengo la mbali.

Ni lengo linaloangaza kukomesha ubaguzi, kuondoa ukatili dhidi ya wanawake, ndoa za kulazimishwa na ukeketaji, kugawana kazi za nyumbani, kuhakikisha upatikanaji wa afya ya ngono au hata kuhakikisha ushiriki mzuri katika maisha ya kisiasa na kiuchumi.

Kila mwaka, takwimu zinataja kuwapo watu milioni 245 wenye umri zaidi ya miaka 15, wanafanyiwa ukatili wa kimwili na wenza wao.

Vilevile inaelezwa, katika kundi hilo kuna ambao wameolewa kabla ya umri wa miaka 18, wanaofanya kazi za nyumbani bila ya malipo.

### HALI ILIVYO LONGIDO

Kupitia Jeshi la Polisi, Kitengo cha Dawati la Jinsia, kumekuwapo jumla ya kesi 239 za ukatili zilizowasiliwa kwa mwaka huu, tofauti na mwaka jana, kumekuwapo kesi 312.

Mchanganuo wa kesi za mwaka huu ni na idadi yake kwenye mabano: Mimba shuleni (48), ubakaji (9), shambulio (161), shambulio la aibu (2), ukatili dhidi ya mtoto (2), kutelekeza familia (1), kumzorotesha mwanafunzi masomo (13), kumwozesha mtoto chini ya umri (1), na kushindwa kutunza mtoto ina kesi moja.

"Kesi 32 watuhumiwa wamefungwa na wengine kulipa faini, kesi moja ipo mahakamani, jumla ya wanafunzi 8,915 wamepata mafunzo ya ukatili wa kijinsia. Wapo wengine waliokolewa kwenye matukio ya ndoa za lazima wamehifadhiwa nyumba salama" anafafanua Ofisa Jinsia Polisi, Kplo Francisca.





# UNFPA yataka vijana wapate huduma rafiki afya ya uzazi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MSAIDIZI wa Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), amewataka vijana kupata taarifa na huduma rafiki za afya ya uzazi, ngono salama, maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na kuzuia ukatili wa kijinsia ili wajilinde na kuwalinda wengine.

Dk. Majaliwa Marwa alitoa rai hiyo jana alipofungua kongamano la Young and Alive Summit 2023 linalofanyika juzi jijini.

Alisema kwa maslahi na ustawi wa taifa, vijana wanatakiwa kuhakikisha wanapata taarifa na huduma rafiki za afya ya uzazi na ngono salama ikiwa ni pamoja na kuzuia ukatili wa kijinsia na maambukizi ya VVU.

Dk. Marwa alisema vijana ni nguzo ya taifa lolote, viongozi wa baadaye, wajasiriamali, waajiri, wanamichezo, wanaochochea maendeleo na nafasi ya vijana hawawezi kuipuuza.

Alisema kuwa kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Tanzania ina watu milioni 61, lakini karibu nusu ya Watanzania wote wako chini ya miaka 18, pia vijana wenye miaka 15 hadi 35 ni theluthi ya watu wote nchini.

Alisema ripoti ya hivi karibuni inaonesha wasichana waliobalehe wenye umri wa miaka 15 na 19 wanakadiriwa asilimia 3.4 wana maambukizi ya VVU ikiwa na mara tatu ya kiwango cha maambukizi kwa vijana wa kiume wenye umri kama huo.

Mkurugenzi Mkuu wa shirika lisilokuwa la kiserikali la Young & Alive, Sesilia Shirima alisema lengo lao ni kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya afya hususani afya ya uzazi kwa makundi ya vijana balehe na vijana kwa ujumla.

"Maoni ya shirika ni kuona Tanzania yenye vijana wenye afya wanaotambua kutumia haki zao za afya ya uzazi na ngono salama wanaweza kujikinga na mimba zisizotarajiwa, maambukizi ya magonjwa ya ngono ikiwa ni pamoja na VVU na kupigania usawa wa kijinsia," alisema

Aliongeza kuwa tangu mwaka 2017, wamekuwa wanafanya kazi ya kukuza afya ya uzazi na ngono salama kwa vijana nchini.

Alisema kongamano hilo linahudhuriwa na vijana 300 kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar wenye motisha na shauku ya kuimarisha afya ya jamii zao kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania.

Ofisa Miradi Kitengo cha Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto kutoka Wizara ya Afya, Edith Senga alisema vijana wamekuwa wanakutana na changamoto mbalimbali. Serikali imekuwa inashirikiana na wadau mbalimbali kutoa elimu ili kukabiliana na kero zinazowakabili.

# RAS akosoa utaratibu wa wizara kuwafuta shule wanafunzi watoro

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIBU Tawala Mkoa wa Singida ameshauri Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuangalia upya sera inayotoa siku 90 mwanafunzi asipohudhuria masomo, anafukuzwa shule kwa kuwa inatumika vibaya na inazalisha watoto wengi wa mitaani.

Dk. Fatuma Mganga, alitoa angalizo hilo juzi wakati wa uzinduzi wa Mpango wa Elimu kwa Vijana Walio Nje ya Mfumo Rasmi (IPASO) awamu ya pili.

Mpango huo utatekelezwa katika mikoa sita ya Singida, Shinyanga, Simiyu, Tanga, Pwani na Manyara kwa ufadhili wa Serikali ya Korea kupitia Shirika la KOICA, ikitoa Dola za Marekani milioni sita.

Alisema sera hiyo imekuwa inatumika vibaya kutokana na baadhi ya wazazi ambao wanaona suala la elimu ni kero kwao kwa kuzuia watoto wao ambao ni wanafunzi wasiende shuleni kusubiri siku 90 zifike ili wafutwe katika shule wanazosoma, hali inayosababisha kuzalisha watoto wengi wa mitaani.

"Hii sera inayosema mtoto akikaa nje ya shule anakuwa amejifuta na anatakiwa kufutwa katika shule anayosoma inatumika vibaya. Ni wakati mwafaka kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuiangalia upya ili mabadiliko ya sheria yaweze kufanyika," alishauri.

Alisema programu ya IPASO ambayo inasaidia kupunguza vijana wa mitaani na kuwafanya kupata ujuzi na hivyo kuwasaidia kujenga uchumi wao na wa taifa kwa ujumla, kwa Mkoa wa Singida vijana zaidi ya 15,000 wanaguswa.

Mwakilishi wa Kamishna wa Elimu, Oscar Msalila, alisema programu ya IPOSA inatekelezwa katika mikoa 10 Tanzania Bara ambayo ni Dodoma, Kigoma, Iringa, Tabora, Mbeya, Dar es Salaam, Njombe, Songwe, Shinyanga na Rukwa.

Alisema kupitia programu hiyo, vijana wenye umri kuanzia miaka 14 wapatao 42,183 wameweza kujengewa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK), stadi za maisha, stadi za ujasiriamali na ufundi stadi ili wajikomboe kiuchumi na kuchangia uchumi wa taifa katika programu ya muda mrefu na mfupi.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Pantalee Kapichi, alisema kuwa mwaka 2015, shirika hilo kama mdau muhimu wa maendeleo lilifadhili utafiti unaohusu hali halisi ya vijana na watoto walio nje na shule na kubaini wako zaidi ya 3,500,000 nchini.

Kapichi alisema katika kuhakikisha kundi hili linafikiwa, UNICEF ilitoa ufadhili kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) ilipewa jukumu la kuandaa programu ya IPOSA ambayo ilizinduliwa kwa mara ya kwanza 2019 mkoani Tabora. Alisema kuwa baada ya uzinduzi huo, UNICEF ilifadhili utekelezaji katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Dodoma na Dar es Salaam na kwamba shirika hilo litaendelea kufanya kazi na serikali kuhakikisha programu inawanufaisha vijana wengi zaidi.

"UNICEF inajivunia kuona ndoto yake ya kuona IPOSA inatekelezwa nchi nzima inaanza kutimia kwani hadi sasa mikoa 16 kati ya 26 imefikiwa kuwezesha watoto na vijana balehe wa kitanzania kupata fursa ya elimu itakayowawezesha kujikwamua kiuchumi," alisema.

Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Watu Wazima na Elimu Maalum kutoka Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ernest Hinju, alisema kuwa kwa sasa serikali ina mpango wa kuangalia namna ambavyo vijana wa makundi maalum wananufaika na programu ya IPOSA.



Wafanyabiashara wakiendelea na shughuli zao katika Soko la Sabasaba jijini Dodoma jana, huku kukiwa na rundo la takataka zilizotelekezwa bila ya kuzolewa kwa takribani wiki ya tatu sasa na kuhatarisha usalama wa afya zao na wateja. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# 'Zingatieni sheria, miongozo ya WB katika mradi miliki za ardhi'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imezitaka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Mkazi na Wizara ya Fedha kuzingatia sheria na taratibu za nchi na miongozo ya Benki ya Dunia (WB) wakati wa kutekeleza mradi wa uboreshaji usalama wa miliki za ardhi (LTIP).

Maagizo hayo yalitolewa juzi na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Slaa, aliposoma hotuba kwa niaba ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwenye mkutano wa kitaifa wa wadau kujadili utekelezaji mradi wa uboreshaji usalama miliki za ardhi.

Alisema kuwa Januari 21, 2022, serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilitia saini makubaliano na Benki ya Dunia ya mkopo wa Sh. bilioni 346 sawa na Dola za Marekani milioni 150 kwa ajili ya utekelezaji mradi huo.

"Mradi huu unatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano na una vipengele vinne ambavyo ni kuongeza usalama wa milki, kuimarisha mifumo ya taarifa za ardhi, kujenga miundombinu ya ardhi na usimamizi wa mradi," alisema.

Alisema mradi huo utatoa fursa mbalimbali katika makundi yote ya kijamii kwa kuzingatia makundi maalum na kuleta usawa wa kijinsia.

"Na kuwezesha wamiliki wa ardhi kumiliki ardhi zao kisheria na hivyo kupunguza migogoro mbalimbali inayohusiana na matumizi ya ardhi hasa ya wakulima na wafugaji pamoja na maeneo yaliyotengwa kwa shughuli maalum," alisema.

Waziri huyo alisema vipengele vya mradi vikisimamiwa vyema, vitaleta mchango mkubwa katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na mazingira katika maeneo mengi.

Pia alisema mradi utaimarisha haki za umiliki ambao utachangia kukuza uwekezaji na maendeleo ya kiuchumi, kuongeza uzalishaji na usalama wa chakula, kupunguza migogoro ya ardhi na kukuza utunzaji wa mazingira.

"Moja ya vitu vikubwa vitakavyofanywa na mradi ni ujenzi wa majengo 25 ya Ofisi za Ardhi za Mikoa, ofisi hizi zote zitawezeshwa kufungwa mfumo wa kielektroniki wa usimamizi na utekelezaji kazi za ardhi.

"Niendelee kuwaagiza wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri zinazotekeleza mradi, kutoa ushirikiano kwa timu za utekelezaji wa mradi.

"Taasisi zinazofanya kazi karibu na mradi zikiwamo NIDA, NEMC, Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, vyuo vya ardhi na taasisi zingine zote zitoe ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji mradi," aliagiza.

Pia alitoa maelekezo kwa wakurugenzi wa halmashauri nchini katika kipindi cha maandalizi ya bajeti ya mwaka 2024/25, watenge fedha kwa ajili ya sekta ya ardhi ili kuendeleza utekelezaji wa mradi katika maeneo yale ambayo mradi haujafika.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Antony Sanga, alisema tangu utekelezaji wa mradi ulipoanza Machi mwaka huu, umepata mafanikio mbalimbali mijini na vijijini.

Alisema mafanikio hayo ni pamoja na kazi za upimaji na umilikishaji ardhi kwa upande wa vijijini unaendelea katika halmashauri tano za wilaya ambazo ni Tanganyika, Mufindi, Maswa, Mbinga na Songwe.

"Hadi kufikia tarehe 20 mwezi huu, wamiliki wa vipande vya ardhi 122,045 wametambuliwa vijijini na tayari hatimilki za kimila 10,568 zimeandaliwa na kusajiliwa katika mfumo wa usimamizi wa ardhi," alibainisha.





# Mfumo mpya takwimu mazao wazinduliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TANZANIA kwa kushirikiana na nchi ya Morocco, imezindua mfumo mpya wa kukusanya takwimu za mazao kwa njia ya kidijitali tangu yakiwa shambani.

Lengo la mfumo huo ni kujua kiwango cha uzalishaji wa kila zao nchini, mradi ambao utalisaidia taifa kujiwekea akiba ya kutosha ya chakula na ziada kuiuza nje ya nchi.

Mtafiti wa Udongo wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, Fedrick Mlowe, ambaye ndiye mratibu wa mfumo huo, alisema takwimu za mazao zitakazokuwa zinakusanywa kwa mfumo huo zitakuwa sahihi.

Alisema hivi karibuni maofisa kilimo wa mikoa 24 nchini walihudhuria mafunzo maalumu ya namna ya kuutumia mfumo huo kwenye ukusanyaji wa takwimu za mazao.

Mlowe alisema takwimu za mazao kabla ya kuanzishwa kwa mfumo huo zilikuwa zikikusanywa kwa kukadiria jambo ambalo lilikuwa linasababisha zisiwe na usahihi kwa asilimia 100.

Alisema mradi huo utasaidia taifa kujua kiwango cha uzalishaji kwa mwaka husika na kuweka ulinganifu na mwaka uliopita pamoja na kuandaa mikakati ya mwaka unaofuata.

"Mfumo huu ni wa kisasa na unakusanya taarifa kwa kutumia satelaiti, unaweza kukusanya taarifa toka mmea unapoanza hatua za ukuaji hadi kuvuna na unauwezo mkubwa wa kukusanya taarifa za mashamba yote yaliyolimwa na yasiyolimwa," alisema Mlowe.

Mtafiti huyo alisema maofisa kilimo hao watapatiwa simu janja ambazo zitatumika katika ukusanyaji wa taarifa hizo na kuzijaza kwenye mfumu husika utakao tunza takwimu hizo zitakazo isaidia serikali kujua kiwango cha uzalishaji wa mazao kwa mwaka husika.

Mlowe alisema mafunzo yamejumuisha maofisa kilimo 120 na wasimamizi 24 ambao wamepata mafunzo hayo kwa ushirikiano na Morocco na serikali ya Tanzania, wanawezeshwa vitendea kazi vya kwenda kuchukua hizo takwimu.

Meneja Mauzo wa Kampuni ya Usambazaji wa Mbolea zinazozalishwa Morocco aina ya OCP, Kefas Sima, alisema wameamua kufanya ufadhili wa mradi huo kutokana na awali kufadhili upimaji wa afya ya udongo ambao umekuwa na mafanikio chanya kwa wakulima.

Alisema mfumo huo umekuwa na matokeo mazuri kwa baadhi ya nchi ambazo zimekuwa zikiutumia kutokana na ukusanyaji wa takwimu sahihi za mazao hivyo kuisaidia serikali kutambua kiwango cha uzalishaji kwa mwaka husika.

Sima alisema mradi huo unafadhili kwa kipindi cha miezi nane ambapo wakulima kwa kiasi kikubwa nchini watakuwa wamekwisha lima mashamba yao na kuvuna na kusaidia kuweza kupata takwimu sahihi za mazao.

"Sasa ila hali ya wataalamu kukadilia mazao yakiwa shambani kwa kuangalia na macho suluhisho lake ni huu mfumo ambao wenyewe utafanya hizo kazi kuanzia ngazi ya mmea kuota hadi wakati wa kuvuna," alisema Sima.

Naye Ofisa Kilimo kutoka mkoa wa Rukwa, Ocran Chengula, alisema wamejifunza namna ya kutumia vifaa vya kukusanya takwimu,ambazo zitasaidia kuhakikisha takwimu za kilimo zinawekwa kwenye mifumo ya tovuti.

Alisema mafunzo yatasaidia kuongeza uhakika wa takwimu watakazokusanya za kilimo kwani awali walikuwa wakikadiria uzalishaji wa mazao uliopo katika mkoa wao.

Ofisa Kilimo wa Mkoa wa Katavi, Paulo Sheyo, alisema mfumo huo utawasaidia kuweza kutambua ukuaji wa mimea shambani na kutambua kama imeshambuliwa na wadudu kisha kuwadhibiti mapema kabla ya kusababisha madhara.

## Vyama ushirika vyashirikishwa ugawaji mbolea

**Na Renatha Msungu,** NYASA

KATIKA kuhakikisha mbolea za ruzuku zinafika karibu na wakulima, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imeendelea kiviwezesha vyama vya ushirika kushiriki katika kusambaza mbolea kwa wakulima.

Kutokana na juhudi hizo, tayari wakulima wa Wilaya ya Nyasa walioko umbali wa zaidi ya kilomita 70, wameanza kunufaika na mpango huo baada ya kuhudumiwa na vyama vya ushirika vya msingi vya Kingerikiti na Tingi ambavyo vimekamilisha taratibu zote za kusambaza mbolea na kuanza utekelezaji kwa kuwafikishia pembejeo hiyo muhimu wakulima.

Chama cha Ushirika cha Kingerikiti tayari kimesambaza mbolea kiasi cha mifuko 2,750 kwa wakulima walio wanachama na wasio wanachama huku chama cha msingi cha Tingi kikiwa kimesambaza kiasi cha mifuko 600 ya aina mbalimbali za mbolea na usambazaji unaendelea.

Hayo yamebainishwa na Meneja wa TFRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Michael Sanga, baada ya kutembelea vyama hivyo na kuvikuta vikitoa huduma kwa wakulima wanaowazunguka.

Alisema mamlaka ilivipatia mafunzo na leseni ya kusambaza mbolea vyama hivyo ambavyo vimekuwa msaada sana katika kuhakikisha wakulima wanapata pembejeo hiyo kwa wakati.

"Habari njema ni kuwa vyama vya msingi vya Kingerikiti na Tingi havina changamoto ya mtaji katika kufanya biashara ya mbolea kama ilivyo kwa vyama vingine vya ushirika, hivyo tunaamini watafikisha bidhaa hiyo sawasawa na mahitaji ya wakulima wa maeneo yao," aliongeza.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Kingerikiti, Samwel Kidunda, alieleza kuwa, chama chao kinajitosheleza na hakina changamoto ya mitaji na kubainisha vitafikisha mbolea kulingana na uhitaji.

Adhma ya serikali ni kuhakikisha mbolea inafikishwa karibu na wakulima na adhma hiyo inaendelea kutekelezwa kwa ushirikiano baina ya Wizara ya Kilimo kupitia TFRA, Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Mohamed Mfaki (wa tatu kulia), akikagua mabomba ya mradi wa maji katika kijiji cha Kwabastola, Kata ya Makole, unaotekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani humo jana. Wa tatu kushoto ni Kaimu Meneja wa RUWASA wa wilaya hiyo, Mhandisi Juma Selemani. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Njombe yaanzisha kampeni dhidi udumavu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Mji Njombe imezindua kampeni maalumu ya kutokomeza udumavu sambamba na kuwakumbusha wananchi kuzingatia lishe bora na siku 1,000 za unyonyeshaji.

Akizungumza na wakazi wa Njombe mjini, Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Mji Njombe, Marselina Mtitu, alisema mkoa una tatizo kubwa la utapiamlo hususani udumavu.

"Kwa Halmashauri ya Mji Njombe asilimia za udumavu zimepanda kidogo kutokana na utafiti wa mwaka 2022 ambao unaonyesha kwa halmashauri ni asilimia 45 lakini kimkoa ni asilimia 50.4," alisema Mtitu.

Alisema kutokana na kupanda kwa takwimu, halmashauri ilichukua hatua kwa kuanza kampeni ya kutokomeza udumavu katika mkoa.

"Kampeni inaendana na kaulimbiu ambayo inasema 'Lishe Yangu Afya Yangu' kwa maana kwamba tukizingatia lishe vizuri hata afya zetu zitakuwa vizuri zinaimarika watoto watakuwa na afya bora," alisema Mtitu.

Alisema kampeni hiyo inakwenda sambamba na kuhamasisha wakinamama kunyonyesha watoto kwa kuzingatia siku 1,000 za mwanzo.

"Tulichokibaini kwenye unyonyeshaji ni kuwa kinamama wengi hawako makini katika kuzingatia ule unyeyeshaji. Walio wengi tukiwauliza hata kwenye vituo vya kutolea huduma afya au kwenye siku za afya na lishe ya kijiji au mtaa, tunakuta wanasema mimi siwezi kunyonyesha hiyo miezi sita bila ya kumpa chochote kwa sababu mtoto analia sana," alisema Mtitu.

Aliongeza kuwa kinamama wengi wanazingatia sana shughuli za kiuchumi kuliko malezi.

"Lakini wao wanaacha moja kwa moja kunyonyesha mwingine anasema anazingatia kazi zaidi na badala yake wanapelekea mtoto anapata matatizo mengine ambayo hakutarajia kuyapata, pengine angenyonyeshwa vizuri mtoto yule hata magonjwa mengine yasingempata," alisema Mtitu.

Baadhi ya wanawake mjini Njombe wanakiri kuipokea kampeni hiyo, walisema utamaduni wao wa kufanya kazi ndio unasababisha kushindwa kuzingatia taratibu za kunyonyesha pamoja na kusimamia familia kupata lishe bora.

"Hii kampeni ni nzuri imekuja wakati sahihi, tutajitahidi kupunguza kufanya kazi nyingi lakini na wababa wabadilike nao wafanye kazi ili na sisi tupate muda wa kulea watoto kweli tunawanyima haki hawa watoto," alisema Mary Kyando.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Njombe Mjini, Enos Lupimo, aliwataka wananchi kulima mboga katika maeneo ya makazi yao na kuzingatia lishe bora yenye mchanganyiko wa makundi yote matano ya chakula.

Naye Diwani wa Viti Maalumu Kata ya Njombe Mjini, Tumaini Mtewa, aliwaomba wanawake mkoani Njombe kutotumia muda mwingi katika kazi na badala yake wajikite katika malezi ya watoto kwa kuzingatia maelezo ya wataalamu wa afya.





## RC apigia debe fursa uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi, Idrisa Kitwana Mustafa, ameitaka jamii kuwa mstari wa mbele katika kuzikimbilia fursa zilizoko katika mkoa wake.

Idrisa alitoa wito huo jana katika mjadala wa kampeni ya mkono kwa mkono iliyofanyika Michazani Mall visiwani hapa huku akibainisha kuwa mkoa huo umebarikiwa kuwa na fursa nyingi za maendeleo katika jamii na nchi kwa ujumla.

Alisema miongoni mwa fursa zilizopo ni utaratibu wa utoaji wa mafunzo kwa vijana sambamba na kutoa mikopo ili kuwafanya vijana kujiajiri na kujiinua kiuchumi.

Alisema fursa ya kutoa mikopo kwa vijana inawafanya kujiepusha na kujiingiza katika mambo yasiyoendeleza nchi na kushindwa kujiendeleza kimaisha.

Pia alisema alisema ujenzi wa miundombinu unaoendelea nchini huzalisha fursa za ajira za kudumu na za muda mfupi kwa wananchi wa mkoa huo, hivyo aliwataka wananchi kuzitumia fursa hizo ili kupunguza utegemezi.

"Ujenzi wa barabara za ndani zinazojengwa zimezalisha ajira nyingi kwa vijana wa mkoa wa Mjini Magharibi tuzitumie fursa hizi ili kulisaidia taifa kutokana na umaskini," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa alisema mkoa huo ndio lango kuu la wawekezaji wanaoingia na ndio unaokusanya fedha nyingi za wafanyabiashara.

Naye Mkurugenzi Mtendaji Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA), Juma Burhan, alisema zaidi ya Sh. bilioni nane zimetolewa kwa wanachi wa mkoa wa Mjini kwa ajili kuwainua kiuchumi.

Pia aliwataka wananchi kurudisha fedha za mkopo kwa wakati kwa manufaa ya wananchi na taifa ili kuendelea kuwapatia wananchi wengine mikopo hiyo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Vuai Yahya Lada, alisema zaidi ya miradi 100 imewekezwa katika mkoa huo kulinganisha na mikoa mengine hivyo fursa nyingi zipo katika Mkoa huu wa Mjini Magharibi.

Baadhi ya wananchi walitoa ushuhuda kwa kupatiwa mikopo inayotolewa na ZEEA, walisema wamenufaika kuendeleza biashara zao na kuajiri wengine pamoja na kurudisha mikopo kwa wakati.

Mjadala huo huhusisha wakuu wa mikoa wa Unguja na Pemba katika kuelekea miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar kuangazia fursa, mbinu na changamoto katika mikoa yao.

# Wataja vikwazo mapambano dhidi ya matukio udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WADAU wa kupambana na matukio ya ukatili wamesema kutokuwapo kwa uwajibikaji katika masuala mbalimbali ikiwamo udhalilishaji, kunasababisha kukosekana kwa haki kwa baadhi ya waathirika wa vitendo hivyo.

Walisema hayo jana walipokuwa wakizungumza katika kongamano la kuadhimisha Siku 16 za Kupambana na Matukio ya Udhalilishaji lililofanyika visiwani hapa.

Kwa mujibu wa wadau hao, licha ya taasisi mbalimbali kuadhimisha Siku 16 za Kupinga Ukatili kwa Wanawake na Watoto, bado kuna changamoto ya uwajibikaji katika ufuatiliaji wa kesi hizo.

Mmoja wa wadau hao, Said Ali, alisema bado kuna changamoto katika kufanikisha mapambano ya vitendo hivyo licha ya serikali kuanzisha mahakama maalum ya kusikiliza kesi hizo.

Alisema kwa vile mahakama hiyo ni lazima jamii kushirikiana na vyombo husika ili kuwatayari kutoa ushahidi na kuwafichua wafanyaji wa vitendo hivyo.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Dk. Salum Suleiman Ali, akiwasilisha mada ya utawala wa sheria alisema katika kufikia malengo yote ya uwajibikaji na utawala bora ni lazima wananchi kusikilizwa na kutoa maoni yao juu ya mambo yanayowahusu.

Alisema kwa wakati huu wananchi na serikali bado tatizo la uwajibikaji, hivyo ni vyema kuandaliwa mifumo ya ushirikishwaji wa masuala mbalimbali ambayo itasaidia kuleta mustakabali mwema kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

Katika utawala wa sheria, alisema lazima watu wote wawe sawa kwa mujibu wa sheria bila ya kuwabagua na kuwanyima haki watu wengine.

Akiwasilisha mada ya sheria ndani ya utawala bora, Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU), Dk. Sikujua Omar Hamdan, alisema ili sheria iwe mzuri lazima itoe haki na jamii kuelewa.

Alisisitiza kuwapo kwa miundombinu imara itakayosaidia jamii kuelewa na kuzijua sheria na bila ya kuzijua sheria mfumo wa upatikanaji haki utakuwa mgumu kwa wanajamii.

Dk. Sikujua alisema kabla ya kuandika sheria, kuna umuhimu wa kukaa na jamii kuieleza ili kuondosha ufinyu wa fikra kuhusu tatizo hilo.

Pia alisema kumekuwa na ushirikishwaji mdogo wa watu katika uandaaji wa sheria hali ambayo alisema inasababisha asilimia kubwa kushindwa kufahamu na kuelewa sheria hizo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar), Asha Abdi Makame, alisema ni vyema kupitia siku 16 kuhakikisha haki inapatikana na kukomesha vitendo vya ukatili na unyanyasaji kwa wanawake na watoto.

Naye Ofisa wa Kusimamia Miradi ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia TAMWA - Zanzibar, Zaina Salum Abdallah, alisema kuna umuhimu mkubwa wa kupatikana kwa sheria bora ya kusimamia ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ili kuimarisha utawala bora.

Alisema kuna sheria nyingi zikiwamo za dawa za kulevya, kuzuia rushwa, uhujumu uchumi na mambo mengine, hivyo ni vyema kwa matukio hayo yakawekewa mikakati imara ikiwamo ambayo itachochea uwajibikaji na kufikia malengo hayo.

Naye Hakimu wa Mahakama ya Mkoa wa Kusini Unguja, Khamis Rashid Khamis, alisema mifumo iliyopo hairidhishi katika kumwandaa mtoto juu ya mmong'onyoko wa maadili, hivyo jamii inahitaji kushirikiana kikamilifu katika kumkuza kimaadili na kumwandalia mazingira yake ya baadaye.



Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe, Dk. Muhammed Ali, akila kiapo katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar jana, baada ya kushinda uchaguzi uliofanyika Oktoba 28 mwaka huu, kutokana na aliyekuwa mwakilishi wa jimbo hilo, kufariki dunia. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Asisitiza matumizi roboti maendeleo viwanda

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, Dk. Mahmoud Alawi, amesema mafunzo ya akili bandia ni muhimu kupatiwa wafanyakazi nchini ili kuendeleza mapinduzi ya nne ya viwanda.

Akizungumza juzi wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uelewa watendaji wa taasisi mbalimbali juu ya teknoloji hiyo, Mbweni mjini Zanzibar, alisema kwa sasa dunia inaelekea kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda na matumizi ya roboti yatahitajika ili kurahisisha utendaji kazi.

Dk. Mahmoud alisema akili bandia ina uwezo wa kufanya kazi nyingi kama binadamu, hivyo teknolojia hiyo itaisaidia serikali hasa katika sekta ya viwanda kutekeleza majukumu yake kwa urahisi zaidi.

Awali, Dk. Mahmoud aliwataka washiriki hao kuwa watulivu na kufuatilia mafunzo hayo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Naibu Mkuu wa Taasisi ya Karume (Taaluma), Dk. Khamis Khalid Said, alisema kukamilika kwa mafunzo hayo kutasaidia kurahisisha utendaji katika maeneo mbalimbali yakiwamo biashara, afya, nishati na uchukuzi.

Pia alisema mafunzo hayo yamefanyika kutokana na ushirikiano mzuri uliopo kati ya Taasisi ya Karume na Chuo Kikuu cha AP cha Ubelgiji kwa lengo la kupata ubunifu na kuboresha utendaji kazi.

Mkufunzi kutoka Chuo Kikuu cha AP, Piric Ven Muoek, alisema katika kuhakiksha mradi huo unafikia malengo, wanafunzi wanne wa chuo hicho watapata fursa ya kuendeleza mafunzo hayo Ubelgiji ili kuiendeleza programu hiyo Zanzibar.

Mmoja wa washiriki, ambaye ni Mkuu wa Programu za Uwezeshaji Wakala wa Uwezeshaji Wananchi kiuchumi, Raya Idrisa Ahmada, alisema mafunzo hayo yanaweza kuleta mabadiliko ya kiutendaji nchini. Aliziomba taasisi zinazohusika na masuala ya viwanda kutoa ushirikiano ili kuendeleza mradi huo hadi kufikia malengo.

Mafunzo hayo yaliwashirikisha wajasiriamali na watendaji wa taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ADELIVA CREMENCE MASEHE**
Anatangaza kupotea Kwa Cheti cha kidato cha Nne chenye Index namba **S4894/0001/2016** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **CANAAN SEKONDARI** mwaka 2016. Kwa yeyote atakayeiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/TAN/MUH/3004/2023**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**SUNDAY STUART DILUNGA** anatangaza kupotelewa kwa hati yangu ya kusafiria yenye namba TAE523792 iliyotolewa makao makuu uhamiaji jijini DAR ES SALAAM. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIG/47336/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**VERONICA LAWRENCE NDUNGURU** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 898 DKY aina TVS STAR. Chassis namba MD625AF4XNIC21810. Engine namba DF4CN1273113. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/ILA/29792/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MURTAZA HUSSEIN BUDHA** anatangaza kupotelewa na kadi ya TRAILER yenye namba za usajili T 122 CQF. Chassis namba NISSA714290290MHB. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/7623/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DOMINICK REMMY NYAMBIGE** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T944DCF KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFIA KITUO CHA KARIBU CHA POLISI TAARIFA:- **PHQ/IRI/MUF/3588/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 63 YA 2023**

**TATU RAJABU MOHAMED (Suing through Power of attorney of FATMA SAID KIBWANA)........MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**JULIUS PETER SHAYO,ABIYA YONA MATHIAS,MUSSA TINDA.............WAJIBU MAOMBI**
**AMINA RAMADHANI SHADA.........NECESSARY PARTY**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**AMINA RAMADHANI SHADA**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza za Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 30/11/2023 mbele ya mwenyekiti M.KHASIM wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilzwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 20 Mwezi November, 2023.

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA MOROGORO**

**KITUO CHA MJINI, MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......124/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: MARTHA LABANI SIJILA WA MADIZINI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MKEGANI HAMISI KIBWANA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 04 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia.

Imetolewa leo tarehe 16 mwezi 11 mwaka 2023

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**
**WILAYA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......26/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: GILLEARD ONAEL MARO WA KIGURUNYEMBE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA RITA ELIAS LYAMUYA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 18 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia.

Imetolewa leo tarehe 20 mwezi 11 mwaka 2023

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BAKARI ALI BANGU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 672 DKL – TATA. Chassis namba MAT751006G8R27043. Engine namba 497TC73NTY842518. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/8244/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JEREMIA SIMON MICHAEL** Anatangaza kupotea Kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya Usajili **T376 BDV.** Kwa yeyote atakayeiona atoe Taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya Polisi: **HAN/B.1/19/VOL9/301**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**SHAURI LA MAOMBI YA UTEKELEZAJI HUKUMU NO. 34/2019**

**TATA AFRICAN HOLDING TANZANIA LTD...........MLETA MAOMBI**

**VERSUS**

**MSAFIRI DEOGRATIUS NKOUBI..............MJIBU OMBI**

**KWA: MSAFIRI DEOGRATIUS NKOUBI**

**POPOTE ULIPO.**
**KUITWA SHAURINI**

ZINGATIA shauri tajwa hapo juu limepangwa kwa ajili ya kutajwa tarehe 01/12/2023 saa 09:30 asubuhi. Mbele ya Mhe. M.O NDYEKOBORA – PRM.

Hivyo mnatakiwa kuhudhuria Mahakamani hapa bila kukosa na kuwasilisha nyaraka zako zote na majibu ambayo mtaona ni vyema na muhimu katika kuthibitisha shauri hilo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na kuwekwa mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 15/11/2023.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI
MWANZA

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0745 700 710.
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Kaunda suti marufuku bungeni Kenya

**NAIROBI,** KENYA

BUNGE la Kenya limepiga marufuku uvaaji wa kaunda suti, kutumika kama vazi rasmi ndani ya chombo hicho cha kutunga sheria.

Vazi lilipewa jina hilo kutokana na kupendelewa kuvaliwa na aliyekuwa Rais wa Zambia marehemu Kenneth Kaunda.

Spika wa Bunge la Kenya, Moses Wetangula, alisema suti za Kaund pamoja na nguo za asili za Kiafrika, hazikubaliki kuvaliwa wakati wa vikao vya bunge.

Rais wa Kenya, William Ruto, mara nyingi huvaa kaunda suti wakati wa hafla rasmi za serikali na kusababisha kupendwa na wanasiasa.

Suti hiyo, ambayo pia inajulikana kama suti ya Mao Zedong, haina ukosi na mara nyingi huwa ya mikono mifupi.

Wetangula alisema uamuzi wake wa kupiga marufuku suti hiyo ulitokana na mitindo iliyoibuka ambayo ilikiuka kanuni za mavazi ya bunge.

Alibainisha kuwa kanuni sahihi ya mavazi kwa wanaume ni kanzu, ukosi, tai, shati ya mikono mirefu, suruali ndefu, soksi, viatu, au sare. Kwa wanawake mavazi rasmi ni yale ya unadhifu.

Alitaja kuwa sketi na nguo zinapaswa kuwa chini ya urefu wa goti na zenye heshima ndizo zinazokubalika.

Suti ya Kaunda ilishawahi kuruhusiwa bungeni na baadhi ya wabunge wamekuwa wakijulikana kwa kuvaa mara nyingi.

Spika Wetangula alikiri kwamba suti hizo zilivumiliwa kwa namna fulani, lakini ni wakati wa kusitisha kutumika.

Suti hiyo ya kaunda imevuma kwenye mitandao ya kijamii nchini Kenya hivi karibuni, baada ya Rais Ruto kuanza kuvalia katika hafla rasmi.

Kupigwa marufuku kwa suti hiyo kumezua hisia tofauti kwenye mitandao ya kijamii, huku wengine wakishangaa ni kwa nini vazi la Kiafrika lizuiwe kuvaliwa ndani ya Bunge.

# Israel na Hamas wazidi kusaka amani muda ukienda ukingoni

**GAZA,** PALESTINA

TAIFA la Israel na kundi la Hamas wameitumia siku ya kwanza ya kurefusha mkataba wa kusitisha mapigano kwa kuendelea kubadilishana mateka na wafungwa.

Matukio hayo yamefanyika katika siku mbili ya ziada ya usitishwaji mapigano, huku hali ya wasiwasi ikiongezeka juu ya nini kitatokea baada ya muda huo kumalizika jana.

Katika siku ya kwanza jana Jumanne, mateka 10 wa Kiisraeli waliachiwa huru na kundi la Hamas. Idadi hiyo inajumuisha wanawake 9 na msichana wa miaka 17.

Mateka walioachiwa huru wakiwamo raia wawili wa Thailand. Kundi hilo la mateka 11 lilikabidhiwa kwa Shirika la Msalaba Mwekundu kabla ya kupokelewa na mamlaka za Israel.

Muda mfupi baadaye, Israel nayo iliwaachia huru wafungwa 30 wa Kipalestina waliokuwa wakishikiliwa kwenye moja ya jela zake.

Tangu kuanza usitishaji mapigano Ijumaa iliyopita kundi la Hamas kwa jumla limewaachia huru mateka 81, wengi wakiwa raia wa Israel.

Kwa upande mwingine Israel nayo imewaachia wafungwa 180 wa Kipalestina.

Katika muda huo wa kusitisha mapigano, umewezesha kuingizwa msaada mkubwa wa kiutu ndani ya Ukanda wa Gaza eneo linalokabiliwa na hali mbaya ya kibinadamu kutokana na mashambulizi ya Israel yaliyoingia wiki ya saba.

Tangu wakati huo, takwimu za mamlaka za Ukanda wa Gaza zinasema zaidi ya watu 14,000 wameuawa kutokana na mashambulizi makali ya ardhi, angani na majini yanayofanywa na vikosi vya Israel.

Israel ilisema dhamira ya operesheni hiyo ni kulitokomeza kundi la Hamas linalotawala Ukanda wa Gaza na ambalo nchi hiyo pamoja na Marekani, Umoja wa Ulaya na mataifa mengine ya magharibi yameliorodhesha kuwa la kigaidi.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alikwishasema kampeni yake ya kijeshi itaendelea baada ya muda wa sasa wa usitishaji mapigano kumalizika.

Akizungumza na kituo cha utangazaji cha Ujerumani, Welt Tv, Netanyahu alisema nchi yake haina chaguo jingine isipokuwa kupambana dhidi ya Hamas na kulitokomeza kundi hilo.

Licha ya matamshi hayo ya Netanyahu, juhudi bado zinafanyika kufanikisha makubaliano mengine ya kurefusha muda wa kusitisha mapigano lakini hakuna juhudi zozote alau kwa hivi sasa za kukomesha kabisa operesheni ya Israel huko Gaza.

Hata hivyo, taarifa zinaeleza kwamba majadiliano yanaendelea nchini Qatar yakiwahusisha viongozi wa mashirika ya ujasusi ya Israel, Marekani na maofisa wa Misri kujaribu kufikia makubaliano mapya ya kusitisha mapigano.

Wakati huo huo misaada zaidi imeendelea kupelekwa Ukanda wa Gaza kuwasaidia raia wanaopitia hali ngumu ya maisha kwa kukosa mahitaji muhimu ikiwamo chakula.

Marekani ilisema imesafirisha kwa ndege zaidi ya tani 50,000 za chakula na vifaa vya matibabu kwenda Gaza. Shehena hiyo ni ya kwanza kati ya awamu tatu za misaada inayotarajiwa kupelekwa Gaza.

Uturuki nayo ilisema itakamilisha hivi karibuni ujenzi wa hospitali za muda ndani ya Ukanda wa Gaza na kuanza kutoa huduma mara moja.

Waziri wa Afya wa nchi hiyo, Fahrettic Koca alisema hayo baada ya ujumbe wa Uturuki kuingia Gaza kupitia mpaka wa Rafah kwa ajili ya kutathmini maeneo yanayofaa kujengwa hospitali hizo.

**DW**



Mfungwa wa Kipalestina aliyeachiwa na Israel akikumbatiana na jamaa yake jana alipowasili ukingo wa Magharibi. **PICHA: XINHUA**

# Msafara wa Katumbi washambuliwa, mmoja auawa, wengi wajeruhiwa

**KINDU,** DRC

KIONGOZI wa chama cha mpinzani mkuu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Moise Katumbi, ameuawa na wengine kadhaa katika vurumai iliyoibuka katika mkutano wa kampeni uliofanyika jana katika mkoa wa Kindu.

Uchaguzi nchini humo umepangwa kufanyika Desemba 20, umekuwa na mvutano mkali kati ya wagombea wawili Rais Felix Tshesekedi na Katumbi kutoka Chama cha Ensemble pour la République.

Tukio hilo limekuwa la kwanza kubwa kutokea katika kipindi cha kampeni ambacho kimeshuhudia upinzani mkali kwa wafuasi wa wagombea hao wawili.

Hali ya mvutano iliripotiwa kabla ya kutua kwa ndege ya Moïse Katumbi, baada ya mamlaka ya mkoa huo kumzuia kufanya mkutano wa kampeni katika eneo maarufu lililoko katika barabara kuu ya mji wa Kindu.

Mara alipowasili, Katumbi na washirika wake, akiwamo Waziri Mkuu wa zamani Matata Ponyo na Seth Kikuni, walishangiliwa na kufuatwa na umati wa watu katika mitaa mbalimbali kabla ya mkutano huo kuhamishiwa sehemu nyingine.

Msafara huo ulipokaribia kukaribia makazi ya mkuu wa mkoa wa Kindu, wafuasi wa chama tawala walimshambulia Katumbi na wanachama wake kwa kurushiwa mawe.

Katika makabiliano hayo, mkuu wa msafara huo, Dido Kakisingi, ambaye ni kiongozi wa vijana wa chama cha Katumbi huko Kindu, alipigwa na kifaa cha kulipuka na kuanguka chini.

Kulingana na taarifa za chama hicho cha upinzani, watu hao walimpiga akiwa chini na kufa papo hapo.

Hata hivyo, Meya wa Kindu, alisema kada huyo wa Chama cha Katumbi alianguka kutoka kwenye gari lililokuwa kwenye msafara wa kiongozi huyo na kukanyagwa na gari lingine.

Alisema polisi waliingilia kati na kufyatua risasi za moto kutuliza ghasia hizo na kusababisha watu kadhaa kujeruhiwa.

HABARI MICHEZO

# DIARRA FITI KUIVAA AL AHLY, BACCA AJIFUNGA YANGA SC

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kipa chaguo la kwanza wa Yanga, Djigui Diarra, akiwa kamili kuikabili Al Ahly katika mechi ya hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, klabu hiyo imempa mkataba mpya wa miaka minne beki wao, Ibrahim Hamadi 'Bacca', ili kuendelea kuitumikia timu hiyo.

Akizungunza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema Diarra ambaye alikosa mchezo wa kwanza wa hatua hiyo dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria na timu hiyo kuchapwa mabao 3-0, hivi sasa amepona na ikimpendeza kocha wao atasimama langoni Jumamosi.

Kamwe alisema kurejea kwa Diarra kunakiongezea nguvu kikosi chao ambacho malengo yake ni kusonga mbele katika michuano hiyo ya kimataifa.

"Taarifa nzuri tuliyoipata kutoka kwa madaktari, Diarra ameimarika na alikuwa kwenye mazoezi na wachezaji wenzake kwa siku mbili, kwa hiyo tunaamini kuelekea katika mchezo dhidi ya Al Ahly, Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, atakuwa na machaguo mengi, ikiwezekana kama itampendeza au ataona ameshakuwa na utimamu wa mwili, basi anaweza kumpanga.

Tunajua uwezo wake na mashabiki wa Yanga wanatamani kumuona akisimama langoni, akirejea katika nafasi yake ya kupambania klabu," alisema Kamwe.

Aliongeza alisema kipa huyo ambaye aliumia bega na ndiyo sababu pia alikosa mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Coastal Union, lakini taarifa hiyo waliificha kwa sababu maalumu.

"Tupo katika Ligi ya Mabingwa Afrika, kila taarifa huwa ni muhimu, hatukuitoa kabla kwa sababu ni kama unampa ahueni mpinzani, anajiandaa kutokana na mapungufu ulionayo, benchi la ufundi lilishauri taarifa kama hizi tuzihifadhi ili kutotoa fursa kwa mpinzani ili kujua taarifa zako za kiufundi kuelekea katika mchezo huu," Kamwe alisema.

Aliongeza maandalizi kuelekea mechi dhidi ya Al Ahly yanaendelea vizuri na wanaamini watapata matokeo mazuri na majukumu yote wamewaachia wachezaji wao.

"Timu inaendelea na mazoezi kama kawaida, tumewapa utulivu wachezaji wajiandae, wajue wana kazi kubwa ya kuifanya siku ya Jumamosi na sisi tunawaambia wao, hawajawahi kutuangusha tunapohitaji jambo letu, naamini tutashinda mechi hiyo," Kamwe aliongeza.

Kuhusu mkataba mpya wa Bacca, Kamwe alisema uongozi umefikia uamuzi huo baada ya kufahamu mkataba wa awali wa beki huyo wa kati unaelekea kumalizika.

"Jana (juzi), tumeboresha mkataba wa beki wetu, Ibrahim Hamad 'Bacca', amepewa mkataba mrefu zaidi katika historia ya mchezo wa mpira wa miguu nchini na wenye thamani kubwa, hii ina maana hata kama akiondoka kwa kuuzwa, klabu itapata kipato kinono zaidi, yupo mpaka 2027," alisema.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania Bara ya umri chini ya miaka 18 wakishangilia bao katika mechi ya hatua ya makundi ya mashindano ya CECAFA U-18 dhidi ya Sudan Kusini iliyochezwa mjini Kakamega, Kenya jana. Sudan Kusini ilishinda mabao 2-1. **PICHA: TFF**

# Sikinde OG yamnasa Mwezingo

**Na Sabato Kasika**

BENDI mpya ya Sikinde Original imeongeza nguvu katika safu yake ya waimbaji kwa kumchukua, Rashid Mwezingo ambaye kwa muda mrefu alikuwa akifanya shughuli za muziki jijini, Mwanza.

Akizungumzia ujio wa Mwezingo, kiongozi wa bendi hiyo, Abdallah Hemba, alisema mwimbaji huyo alitambulishwa rasmi katika onyesho la bendi hiyo lililofanyika jijini Dar es Salaam Jumamosi iliyopita.

"Ujio wa Mwezingo utaifanya bendi yetu kuwa na waimbaji sita ambao ni pamoja na mimi, Benovilla Anthony, Sharapova, Tabu Mambosasa na Papaa Fanny," alisema Hemba.

Aliongeza bado wanaendelea kuisuka bendi yao na endapo atapatikana mwimbaji mwingine mwenye kipaji watamchukua ili kuendelea kuongeza nguvu.

"Bendi yetu kwa sasa inatamba nyimbo kadhaa zikiwamo za Moyo, Mchepuko, Serengeti, Hila za Ndugum, Mukhtasari wa Kikao na sasa tunajiandaa kufanyia mazoezi wimbo wa Pua ya Nguruwe," alisema.

Kiongozi huyo aliongeza yeye na baadhi ya wasanii wenzake waliamua kujiengua kutoka Mlimani Park na kuanzisha Sikinde Original kwa lengo la kufanya kazi ya kutoa burudani ya kiwango cha juu.

Naye Mwezingo alisema alikuwa nje ya Dar es Salaam kwa muda mrefu lakini sasa ameamua kurejea jijini na kujiunga na bendi hiyo ili kuwapa burudani mashabiki wake.

# JKT TZ yaishtukia Singida FG, yajipanga

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Coastal Union kuchapwa mabao 2-1, kikosi cha JKT Tanzania kimeingia kambini haraka kwa ajili ya kujiwinda na mechi ya raundi ya 12 ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Singida Fointain Gate utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Liti, Singida.

Mbali na ushindi, Singida FG inaonyesha kiwango bora katika mechi zake za hivi karibuni, ikishinda mechi zake tatu mfululizo, mabao 3-1 dhidi ya Mashujaa FC, mabao 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji kabla ya ushindi wa mechi ya juzi.

Ofisa Habari wa JKT Tanzania, Masau Bwire, alisema baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Ihefu Jumapili iliyopita, waliwapa mapumziko vijana wao na baadaye wakaanza mazoezi ya kawaida, lakini sasa wameingia kambini kwa sababu wanajua watakutana na mpinzani mgumu.

Masau alisema JKT Tanzania itaingia katika mechi hiyo kwa tahadhari lakini hawaihofii Singida FG kwa kuangalia matokeo ya michezo yake iliyopita.

"Benchi la ufundi limeanza kutazama ni wapi ambapo tuliteleza katika mechi yetu iliyopita, sisi hatuna wasiwasi na wala hatuihofii Singida, ila tunajua ni timu nzuri, ina wachezaji wazuri lakini timu yetu ina kikosi chenye wachezaji bora kabisa na wala haitashangaza Ijumaa tukawapa kipigo cha kizalendo huko huko kwao," alisema Masau.

Wakati timu hizo zikienda kucheza mechi hiyo, JKT Tanzania inakamata nafasi ya saba ikiwa na pointi 15 kwa mechi 11 ilizocheza, ikishinda nne, sare tatu na kupoteza nne, huku Singida FG ikiwa katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo kibindoni ikiwa na pointi 18, ikishinda mechi tano, sare tatu na kupoteza tatu.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena Jumapili kwa Namungo kuwakaribisha Dodoma Jiji FC kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani, Lindi.

Yanga ndio vinara ya ligi hiyo yenye timu 16 wakiwa na pointi 24 wakifuatiwa na Azam FC iliyojikusanyia pointi 22 huku Simba ikifuata na pointi 19, ikiwa na mechi mbili mkononi.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**ARSENAL: RAMSDALE HAONDOKI**
KLABU ya Arsenal iko tayari kumwachia kipa wa England, Aaron Ramsdale, kuondoka mwishoni mwa msimu huu, lakini hawatamruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 kuondoka wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari. **(90min)**

**CHELSEA YAMKATALIA BROJA**
CHELSEA haitakubali ombi la Fulham la kutaka kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Albania, Armando Broja, mwenye umri wa miaka 22 ifikapo Januari. **(Evening Standard)**

**BEEK KUONDOKA UNITED**
KIUNGO wa Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 26 amesema ataondoka Manchester United ifikapo Januari ikiwa hataanza kucheza mechi nyingi zaidi, akifichua uhamisho wa kuelekea Real Sociedad haukufaulu. **(Diario AS, kupitia Sky Sports)**

**UNITED KUSAKA WAPYA**
KLABU ya Manchester United inatumaini kuimarika katika nafasi nne Januari, ikiwa ni pamoja na safu ya ulinzi huku kukiwa na wasiwasi wa mchakato kuhusu kiungo wa Morocco, Sofyan Amrabat mwenye umri wa miaka 27. **(Guardian)**

**VARANE NJIA PANDA**
BEKI wa Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 30 na kiungo wa kati wa England, Mason Mount (24), ni miongoni mwa wachezaji wa Manchester United walio katika hatari ya kubadilishwa. **(Gurdian, via Express)**

**BAYERN YAMTAKA VARANE**
KLABU ya Bayern Munich imejadili uwezekano wa kumsajili, Raphael Varane kutoka Manchester United lakini hawaoni kama majadiliano hayo yatazaa matunda. **(Sky Germany)**

**WHARTON ANUKIA SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur inavutiwa na kiungo wa kati wa Blackburn Rovers, ambaye ni raia wa England, Adam Wharton, mwenye umri wa miaka 19. **(90min)**

**MUDRYK KUMBEBA SUDAKOV**
MSHAMBULIAJI wa Ukraine na Chelsea, Mykhailo Mudryk, mwenye umri wa miaka 22 anataka klabu hiyo kumsajili mchezaji mwenzake wa zamani wa Shakhtar Donetsk, Georgiy Sudakov (21), katika dirisha la uhamisho la Januari huku wawili hao wakionyesha ushirikiano mkubwa wakati walipokwenda kutumikia taifa lao. **(Gazzetta dello Sport)**

**COTCHER AJIFUA ARSENAL**
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya England ya umri chini ya miaka 17, Mason Cotcher, amekuwa akifanya mazoezi na kikosi cha kwanza cha Arsenal baada ya kuondoka Sunderland. **(Telegraph)**

**WERNER: NITAPAMBANA LEIPZIG**
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner, mwenye umri wa miaka 27 yuko tayari kubakia RB Leipzig na kupigania nafasi yake katika kikosi cha kwanza badala ya kuhamia Manchester United ifikapo Januari. **(Metro)**

**LAZIO KUIKAMUA UNITED**
MANCHESTER United inavutiwa na mlinda mlango wa Lazio, Ivan Provedel, mwenye umri wa miaka 29, lakini klabu yake inayoshiriki Serie A itamuuza Mtaliano huyo kwa pauni milioni 30 pekee. **(Il Messaggero, via Football Italia)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ANCELOTTI: SIWEZI KUSEMA LOLOTE SASA

●●● Ni kuhusu hatima yake ya kubakia au kuondoka Madrid...

**MADRID, Hispania**

WAKATI vita kati ya Real Madrid na Shirikisho la Soka la Brazil (CBF) kuwania huduma ya Carlo Ancelotti ikiendelea kupamba moto, Mtaliano huyo amekataa kuhusishwa kwa jambo lolote.

"Nitakupa nafasi ya kuuliza swali lingine," Ancelotti alimwambia mwandishi wa habari katika mkutano wake na wanahabari kabla ya mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Napoli, alipoulizwa kama atakuwa katika klabu hiyo kwa msimu mwingine.

"Ninasema tena, sizungumzii juu ya maisha yangu ya baadaye."

Huku mkataba wake na ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu, Rais wa CBF, Ednaldo Rodrigues, akitoa kelele za kujiamini kuhusu kumnasa Mtaliano huyo mwenye umri wa miaka 64, Real Madrid wanahaha kumshikilia kocha huyo.

Ofisa mmoja wa klabu hiyo alithibitisha kwa Reuters, Rais wa Madrid, Florentino Pérez, anafikiria kumwongezea mkataba, huku Mkurugenzi wa CBF aliiambia Reuters wanatarajia naye kwa ajili ya mashindano ya Copa América mwaka ujao huko Marekani.

CBF inatarajia kumnasa rasmi Ancelotti ifikapo katikati ya Januari, mwakani na kubatilisha kipengele cha kumalizia mkataba wake na Real Madrid kwa mwaka mwingine na kusema wana "ulinzi wa kisheria" kulinda maslahi yao endapo dili hilo litasambaratika.

"Rais (Ednaldo Rodrigues) hangemsajili Fernando Diniz kwa mkataba wa mwaka mmoja katika nafasi ya uangalizi kama hangekuwa na mpango madhubuti," ofisa huyo wa CBF aliambia Reuters.

"Hakuna kilichobadilika katika nafasi ya rais tangu alipozungumza na vyombo vya habari mara ya mwisho. Mpango ni Carlo Ancelotti na tuko vizuri sana na tunajiamini kwa kujitolea tulionao kufanikisha hilo."

Rodrigues aliiambia Reuters Machi, mwaka huu kumsajili Ancelotti kungekuwa "mtu asiye na akili", na mwezi Julai, wakati wa kumtambulisha mlezi Diniz, aliendelea kujiamini: "Ancelotti atakuwa hapa, unaweza kuwa na uhakika," alisema.

HABARI MICHEZO

# FODEN: CITY TUNAWEZA KUBEBA MATAJI 3 TENA




**MANCHESTER, England**

PHIL Foden amesema Manchester City wana mwelekeo wa kurudia ushindi wa kihistoria wa kutwaa mataji matatu kama ilivyokuwa katika msimu uliopita.

Mchezaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 23 alifunga bao moja na kutengeneza mengine mawili wakati City wakiibuka na ushindi wa magoli 3-2 dhidi ya RB Leipzig na kujihakikishia nafasi ya kwanza katika Kundi G kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ingawa msimu wa 2022/23 daima utakuwa na nafasi maalum katika historia ya klabu, Foden amesisitiza vijana wa Pep Guardiola wanaweza kurudia mafanikio hayo.

Akizungumza na LiveScore, alisema: "Mwaka jana ulikuwa na mafanikio makubwa kwetu, lakini tumedhamiria kurudia tena.

"Hicho ndicho ninachokipenda kwa hawa vijana, hatukariri tulichokifanya mwaka jana, kimepita sasa.

"Tulipofanya hivyo, ilikuwa hisia ya kushangaza. Mara tu tunaposhinda kitu, tunasherehekea kama timu na sote tunataka hisia hiyo tena."

Foden hakukwepa ukweli mabingwa hao wa Ulaya walikosa viwango vyao vya kawaida katika kipindi cha kwanza cha kukatisha tamaa kwenye Uwanja wa Etihad.

Bao la kujifunga la Lois Openda liliifanya Leipzig kuwa mbele kwa mabao 2-0 katika kipindi hicho, jambo ambalo liliamsha maneno makali kwenye chumba cha kubadilishia nguo.

"Kwa upande wa mpira, tuliutoa kwa bei nafuu na tulisema wakati wa mapumziko kwamba tutalazimika kuuweka vizuri zaidi.

"Tunajua tunahitaji bao moja tu Etihad kwa sababu rekodi yetu ya nyumbani ni nzuri.

"Tulipopata la kwanza, umati ulikuwa mkubwa sana. Walikuja nyuma yetu na ilionekana kubadili mdundo mzima wa mchezo."

# Sare ya PSG yamkera Howe

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA Eddie Howe alisema alilazimika "kujidhibiti" baada ya matarajio ya Newcastle United kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kupata shida kubwa wakati Kylian Mbappé alipofunga penalti yenye utata dakika ya 98 na kupata sare ya 1-1 kwa Paris Saint-Germain huko Parc des Princes.

Mwamuzi, Szymon Marciniak, aliyechezesha Fainali ya Kombe la Dunia 2022, alitoa penalti hiyo kufuatia kuingilia kati kwa VAR baada ya mpira kugonga mkono wa beki wa Newcastle, Tino Livramento, kwa krosi iliyopigwa na Ousmane Dembélé.

Hapo awali mpira ulikuwa umegonga kifua cha Livramento kabla ya kugonga mkono wake, lakini Marciniak alitoa penalti hiyo baada ya kukagua tukio hilo kwenye VAR.

Howe aliuita "uamuzi mbaya" lakini akasema Newcastle lazima bado waamini wanaweza kufuzu kwa hatua ya 16 bora.

"Ndiyo ninakubali," Howe alisema, alipoulizwa kama alihisi ukosefu wa haki katika uamuzi huo.

"Kwa maoni yangu sio uamuzi sahihi. Ulikuwa uamuzi mbaya na muda mfupi sana uliobaki, lakini hakuna tunachoweza kufanya nao sasa.

"Lazima nijidhibiti, hiyo ni kazi yangu. Haifai kitu kupoteza udhibiti wa kile unachofikiri na kusema."

Newcastle bado wanaweza kufuzu kwa awamu ya mtoano ikiwa wataifunga AC Milan katika uwanja wa St James' Park na PSG wafungwe ugenini dhidi ya vinara wa Kundi F Borussia Dortmund.

# Upasuaji kumweka Gavi nje miezi 10

**BARCELONA, Hispania**

KIUNGO wa kati wa Barcelona, Gavi anatarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa muda wa miezi nane hadi 10 baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti hapo juzi, kwa mujibu wa ESPN.

Gavi mwenye umri wa miaka 19, aliumia goti wakati akiichezea Hispania dhidi ya Georgia wiki iliyopita.

Hatakuwapo msimu uliobaki akiwa na Barca na pia ataikosa Euro 2024 akiwa na Hispania msimu ujao wa joto, huku michuano hiyo ikitarajiwa kuanza Juni 14, mwakani nchini Ujerumani.

"Gavi amefanyiwa operesheni iliyofaulu kwenye goti lake la kulia lililochanika pamoja na mshono," taarifa ya Barca ilisema juzi.

"Alisimamiwa na daktari wa klabu, Joan Carles Monllau wakati wa upasuaji huo katika Hospitali ya Barcelona."

Kocha wa Barca, Xavi Hernández, alisema wiki iliyopita Gavi, ambaye alishinda tuzo ya mchezaji bora kijana wa Ulaya 'Golden Boy' mwaka 2022, hawezi kubadilishwa kwa sababu ya "moyo, shauku na ujasiri."

Gavi amekuwa mchezaji wa muhimu wa Barca na Hispania msimu huu, alikosa mechi mbili pekee, zote kwa klabu yake kutokana na kusimamishwa.

Wakati wa jeraha lake, ni Marc-André ter Stegen na Ilkay Gündogan pekee waliokuwa wameichezea Blaugrana dakika nyingi zaidi.

Kwa jumla, ameichezea Barca mechi 111 na tangu alipoanza kucheza mechi yake ya kwanza akiwa na umri wa miaka 17 mnamo Agosti, 2021, hakuna mchezaji ambaye ameichezea klabu hiyo michezo zaidi.

Ukali wa jeraha lake umesikika kote Hispania, na chanzo kiliiambia ESPN Rais wa Real Madrid, Florentino Pérez, alikuwa miongoni mwa watu waliomtumia kiungo huyo ujumbe wa kumtakia heri.

Barca ilirejea uwanjani bila Gavi na kutoka sare ya 1-1 na Rayo Vallecano Jumamosi na kumenyana huku juzi iliifunga FC Porto mabao 2-1 katika Ligi ya Mabingwa ya UEFA na kufuzu hatua ya 16 bora kwa mara ya kwanza tangu 2021.

Xavi ametiwa nguvu na kurejea kwa viungo Pedri na Frenkie de Jong katika wiki za hivi karibuni, huku nahodha, Sergi Roberto pia akiwa fiti.

HABARI MICHEZO

# YANGA YAPEWA HAULUNG, SIMBA KUIVAA TEMBO FA

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Kombe la FA, Yanga wamepangwa kukutana na Haulung ya Njombe katika hatua ya 32 bora ya michuano hiyo huku mtani wake Simba akitarajia kuwaalika Tembo FC kutoka mkoani Tabora.

Katika droo hiyo iliyofanyika Dar es Salaam inaonyesha vigogo hao mechi zao zitachezwa jijini.

Singida Fountain Gate watawakaribisha Arusha City kwenye Uwanja wa CCM Liti ulioko mkoani Singida, Dodoma Jiji FC yenyewe itacheza dhidi ya Magereza Dar kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma na Ihefu FC watakuwa nyumbani kuwaalika Rospa FC kutoka Mtwara kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali.

Maafande wa JKT Tanzania wataivaa Mkurugenzi FC ya Simiyu, Namungo FC itakuwa nyumbani dhidi ya Hollywood, Coastal Union itawaalika Green Land kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani, Tanga huku Mashujaa FC wakiwa nyumbani Kigoma dhidi ya Mbuga FC kutoka Mtwara.

Geita Gold FC itakuwa mwenyeji wa Singida Cluster wakati Mtibwa Sugar watawakaribisha Nyakagwe FC ya Geita, ACA Eagle itawafuata KMC kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na Kagera Sugar itacheza dhidi ya Dar City, Azam FC watawaalika Alliance FC ya Mwanza wakati Tabora United itawavaa Minduli Coffee na Tanzania Prisons itachuana na TRA Kilimanjaro. Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Baraka Kizuguto, alisema hatua hiyo itafanyika kuanzia Desemba 13 hadi 17, mwaka huu.

"Mechi zinaweza kuchezwa kuanzia Desemba 13 na kuendelea kulingana na viwanja kwa timu ambazo zinakuwa nyumbani, timu zinatakiwa kufanya maandalizi mazuri kwa sababu bingwa wa Kombe la FA ataenda kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika," alisema Kizuguto.

Mwakilishi wa Yanga, Hafidh Saleh, alisema wanajiamini na kwa sababu hawamfahamu mpinzani wao, watajipanga kupambana kwa ajili ya kusaka ushindi na kusonga mbele.

Naye mwakilishi wa Simba, Hamis Kisiwa, alisema Simba inathibitisha itaingia katika michuano hiyo kwa kucheza soka la ushindani kwa sababu wanataka kulibeba kombe hilo.

"Licha ya kupitia mambo magumu, sasa tumerejea kivingine na tutakuwa tayari kwa ajili ya kusaka ushindi katika mchezo huo na kuvuka hatua hii, kusonga hatua inayofuata," alisema Kisiwa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama, akiwaongoza wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), kucheza muziki wakati wa kufunga kongamano la miaka 36 ya chama hicho lililofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ruvu Shooting FC hoi Championship

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Ruvu Shooting ambayo ilishuka daraja msimu uliopita kutoka Ligi Kuu iko katika hali mbaya kutokana na kuburuza mkia katika msimamo wa Ligi ya Championship ikiwa haijashinda mechi hata moja.

Lakini pia ndio timu inayoongoza kwa kuruhusu kufungwa mabao mengi katika ligi hiyo.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa jana na Bodi ya Ligi, Ruvu Shooting imeruhusu mabao 26 katika mechi 12 ilizocheza ikiongoza kufungwa mabao mengi.

Mabingwa wa Tanzania Bara mwaka 1967, Cosmopolitan inafuatia kwa kuruhusu mabao mengi, imefungwa magoli 19 wakati Copco yenyewe ikiruhusu mabao 18, Trasit Camp mabao 17 na Pan African imetikiswa nyavu zake mara 16.

Takwimu zinaonyesha vinara wa Ligi ya Champioship kwa sasa ni KenGold yenye pointi 26, ikiwa imefunga mabao 20, ambayo ni mengi ukilinganisha na timu nyingine, Mbeya Kwanza iliyo nafasi ya pili kwa pointi hizo hizo 26, inashika nafasi ya pili ikiwa na mabao 19, sambamba na Mbuni FC yenye idadi hiyo ya mabao lakini ipo kwenye nafasi ya tano na pointi zake 21.

Timu za Pamba na Biashara United zote zina mabao 17 ya kufunga, ingawa Pamba inashika nafasi ya nne na pointi zake 24 na Biashara United ni ya sita ikiwa na pointi 21.

## Wachezaji Simba SC wawekwa kitimoto

INATOKA UK. 24

zuri katika michuano yote wanayoshiriki anasisitiza ushirikiano na kujituma kwa wachezaji na viongozi ndio kutafanikisha mipango na malengo yaliyopo.

Alisema pia anahitaji wachezaji wanaojitoa wakati wote na amejipanga kuwapa mbinu zitakazowasaidia kupandisha viwango vyao na kupata matokeo chanya katika kila mechi watakayocheza.

"Ushirikiano ni kitu muhimu kuelekea safari ya mafanikio, ninataka kuona kila mchezaji anapambana na anajitoa kwa ajili ya timu, hii ndio sababu iliyopelekea kuwaita mmoja, mmoja na kuwapa mipango yangu," Benchikha alisema.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi cha timu hiyo kinatarajia kuondoka nchini kesho kuelekea Botswana kwa ndege maalumu ya kukodi.

Ahmed alisema maandalizi ya safari hiyo yamekamilika na wanafahamu wanaenda kukutana na Jwaneng Gallaxy ambayo ilianza hatua hiyo kwa kuifunga Wydad Casablanca bao 1-0 na hivyo kuongoza kundi lao.

## Twiga Stars karata muhimu WAFCON

INATOKA UK. 24

engeneza timu imara itakayoleta ushindani mkubwa wa kupambana ili kupata matokeo mazuri katika mchezo huo.

Nahodha wa Twiga Stars, Oppa Clement, alisema wamejiandaa vizuri na wanaenda kupambana uwanjani kwa kufanyia kazi maelekezo ya benchi la ufundi ili kupata ushindi.

"Kila mchezaji anahitaji kucheza hizi fainali, hali hiyo tunalazimika kupambana, tuna deni kubwa la kuhitaji kucheza fainali hizo, hakuna presha yoyote kuelekea mchezo huu kwa sababu tulishakutana na timu kubwa na kuziondoa.

Kikubwa Watanzania watuombee dua, kazi iliyobaki ni kwetu kuhakikisha tunaenda kutafuta ushindi na kwenda kucheza fainali za WAFCON," alisema Oppa.

Mara ya mwisho na ya kwanza Twiga Stars ilicheza fainali za WAFCON mwaka 2010, ikiwa chini ya Boniface Mkwasa, fainali hizo zikifanyika Afrika Kusini.

Michezo
Alhamisi Novemba 30, 2023
Nipashe



Ancelotti: Siwezi kusema lolote sasa UKURASA 21



Kocha Mkuu wa Simba (katikati), akizungumza na wachezaji wa timu hiyo kwa mara ya kwanza baada ya kujiunga na kikosi hicho kinachotarajia kuelekea Botswana kesho ili kuwafuata wenyeji wao, Jwaneng Galaxy kwa ajili ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: SIMBA SC**

# WACHEZAJI SIMBA SC WAWEKWA KITIMOTO

●●●Ni mkakati wa Benchikha kuweka mambo sawa, yakodi ndege...

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha anaweka mambo sawa sawa, Kocha Mkuu mpya wa Simba, Abdelhak Benchikha, amekutana na wachezaji wa timu hiyo na kufanya nao mazungumzo yenye lengo la kuwajenga na kuwaweka tayari na mapambano katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki, imefahamika.

Simba iliyoko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara inashiriki hatua ya makundi ya michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na mashindano ya Kombe la FA.

Wekundu wa Msimbazi pia mapema mwakani inatarajiwa kuchuana katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi yatakayofanyika Visiwani Zanzibar.

Benchikha aliamua kukutana na wachezaji kwa kuzungumza nao mmoja mmoja ili kuwafahamu kwa karibu kabla ya kuanza kazi rasmi kibarua cha kukinoa kikosi hicho ambacho kesho kitasafiri kuelekea Botswana kuwafuata Jwaneng Gallaxy kwa ajili ya mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

Benchikha alitumia siku ya jana kuzungumza na nyota hao wa Simba na anaamini mazungumo hayo yatamrahisishia kuwaandaa wachezaji kisaikolojia na kuwa tayari kupokea mafunzo ya kiufundi na kimbinu kwenye uwanja wa mazoezi.

Akizungumza na Nipashe jana, Benchikha alisema amekubali kujiunga na Simba kwa sababu anaamini ataweza kuirejesha katika hali yake ya ushindani na kufikia hatua hiyo ni lazima apate muda wa kuzungumza na kila mchezaji peke yake.

Kocha huyo alisema anafahamu Simba ni timu kubwa na kwa ushirikiano wa pamoja watafikia malengo ya klabu hiyo.

"Nipo tayari kufanya kazi na yoyote ambaye anajituma na kipindi hiki nitakuwa naangalia mchezaji mmoja mmoja katika kila nafasi ili kwenda sambamba na maelekezo yangu.

Ninafahamu timu haipo katika hali nzuri kwa sasa, lakini naamini kwa pamoja tutaweza kurejesha heshima ya timu, mimi ni mpambanaji na siogopi changamoto, nipo hapa kuifanya Simba kuwa timu bora na kutwaa mataji," alisema Benchikha.

Kocha huyo raia wa Algeria aliongeza anataka kufanya vi-

INAENDELEA UK. 23

## Twiga Stars karata muhimu WAFCON

**Na Saada Akida**

USHINDI lazima. Hii ni kauli iliyotolewa na benchi la ufundi pamoja na wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), kuelekea mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (WAFCON), dhidi ya Togo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Twiga Stars na Togo zitarudiana wiki ijayo na mshindi wa jumla atapata tiketi ya kucheza fainali zijazo za WAFCON zitakazofanyika Ivory Coast mapema mwakani.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, alisema matayarisho yote yameenda vizuri na amekiandaa kikosi chake kutokana na timu wanayokutana nayo.

Shime alisema anafahamu wanakwenda kukutana na timu ambayo mwaka uliopita walicheza fainali hizo na iko vizuri lakini kwa upande wake wako tayari kusaka ushindi katika uwanja wa nyumbani.

"Tumetoa maelekezo kwa wachezaji kuwa makini katika kujilinda, kutoruhusu bao na kuhakikisha tunatumia vizuri nafasi zitakazopatikana, tumejiandaa kimbinu na kiufundi.

Wachezaji wataenda kutafsiri vizuri kulingana na maelekezo tuliowapa wakati wa mazoezi. Muda mrefu tumejipanga na kurudi katika makali yetu na tuko tayari, kwa maandalizi na wachezaji wa kizazi kipya lakini matumaini yangu kufanya vizuri.

Ukiangalia katika timu nane bora katika michuano ya Olimpiki, Twiga Stars ni miongoni, hii inadhihirisha soka la Tanzania limekuwa zaidi, tumejipanga kucheza na kufanya vizuri," alisema Shime.

Alisisitiza Watanzania wanatakiwa kujitokeza uwanjani kuisapoti timu yao, kwa sababu wamet-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >